**27 JUNI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### Kikao cha Hamsini na Tano – Tarehe 27 Juni, 2025

*(Bunge Lilianza Saa 8.30 Mchana)*

### D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi. *(Makofi)*

Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

### TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Ibara ya 91(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kanuni ya 36(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ninapenda kuwajulisha kwamba leo siku ya Ijumaa tarehe 27 Juni, 2025, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan atalihutubia Bunge katika kuhitimisha uhai wa Bunge hili la Kumi na Mbili ambapo shughuli zake zitafungwa rasmi leo. *(Makofi)*

Ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka Bunge hili la Kumi na Mbili lilifunguliwa rasmi Ijumaa ya tarehe 13 Novemba, 2020 na

Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ambapo alilihutubia Taifa kupitia Bunge. Rais wa Awamu ya Tano alijitambulisha kwa falsafa yake ya Hapa Kazi Tu. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aendelee kumpumzisha kwa amani, Amina.

Waheshimiwa Wabunge, aidha, kufuatia kifo cha Rais wa Awamu ya Tano, Rais wa Awamu ya Sita, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mara baada ya kuapishwa alilihutubia Taifa kupitia Bunge siku ya tarehe 22 Aprili, 2021 kwa kueleza mwelekeo wa Serikali yake wa kudumisha mazuri ya awamu zilizopita, kuendeleza mema yaliyopo, na kuleta mengine mapya kupitia falsafa yake ya Kazi Iendelee.

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyofahamu siku kama hii huwa tunaalika wageni mbalimbali ili kushuhudia tukio hili la Kitaifa, na kama ambavyo mtakumbuka jana tulitengua Kanuni zetu za Bunge ili kuwawezesha wageni hao kuingia ukumbini. Kwa muktadha huo nitasitisha Shughuli za Bunge kwa muda ili niruhusu wageni wetu waanze kuingia ukumbini na mimi nitaenda kumpokea Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wakati wageni wetu wakiingia ukumbini wote mnakumbushwa kuendelea kutulia katika viti vyenu. *(Makofi)*

Sasa baada ya kusema hayo ninasitisha Shughuli za Bunge mpaka muda mfupi ujao.

*(Saa 09.02 Alasiri Bunge Lilisitishwa kwa Muda)*

**NDG. PATSON SOBHA – MSHEREHESHAJI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Tume ya Utumishi wa Bunge, Kamati ya Uongozi ya Bunge, Waheshimiwa Wabunge na wageni waalikwa; ninaanza kutangaza utaratibu wa misafara ambayo itaingia hapa ndani kama Spika alivyosema kwamba amekwenda kumpokea Mheshimiwa Rais, lakini kuna misafara

ambayo itaingia hapa na msafara wa mwisho utakuwa ni wa Mheshimiwa Rais akiwa ameongozana na Mheshimiwa Spika.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sasa ninatangaza tu, bado hawaingii lakini msafara wa kwanza kabisa utakuwa umetanguliwa na Mpambe wa Bunge, utafuatiwa na viongozi wafuatao; Mwenyekiti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, akifuatiwa na Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mheshimiwa Alhaj Zubeir Ali Maulid, na kisha Spika wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mheshimiwa Joseph Ntakarutimana, na Makatibu Mezani watatu; Ndugu Monica Mwaga, Ndugu Pili Omari na Ndugu Emmanuel Mpanda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, msafara wa pili utatanguliwa na Mpambe wa Bunge na kufuatiwa na Mwenyekiti wa Bunge, Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, na kisha Jaji Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa George Mcheche Masaju, na nyuma yao Makatibu Mezani watatu; Ndugu Michael Chikokoto, *ndc;* Ndugu Aziza Makwai na Ndugu Mkuta Masoli. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, msafara wa tatu utatanguliwa na Mpambe wa Bunge pia, lakini kiongozi atakayekuwa amefuatia ni Mwenyekiti wa Bunge, Mheshimiwa Kizito Joseph Mhagama, atafuata Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, na kisha Makatibu Mezani watatu; Ndugu Yona Kirumbi, Ndugu Bakari Kishoma na Ndugu Zainab Issa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, msafara wa nne utatanguliwa pia na Mpambe wa Bunge, na kufuatiwa na viongozi wafuatao; Naibu Spika wa Bunge, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu; Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi; na Makatibu Mezani watatu; Ndugu Ruth Makungu, Ndugu Athuman Hussein, *ndc* na Ndugu Asia Minja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kisha msarafa wa tano ambao nimesema ndiyo wa mwisho, utatanguliwa pia na Mpambe wa Bunge, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, akiwa ameongozana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, na kisha Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard na Makatibu Mezani wawili; Ndugu Aziza Waziri Kheir, pamoja na Ndugu Joshua Chamwela, *ndc. (Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Wabunge, huu ni utaratibu wa makundi. Nikipewa ishara ya kutangaza sasa makundi yaingie nitarudia tena kutangaza kama ambavyo nimefanya. *(Makofi)*

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walisubiri kwa muda ili wageni waliotajwa waweze kuingia Ukumbini)*

**NDG. PATSON SOBHA – MSHEREHESHAJI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa bado sijaambiwa ninaomba nitoe matangazo mengine likiwepo la utaratibu wa kupiga picha.

Waheshimiwa Wabunge mtasalia hapa wakati viongozi wote wakitoka, ile misafara ambayo nitaitangaza wakati wa kutoka. Ikishatoka Waheshimiwa Wabunge bado mtaendelea kubaki kwa sababu ya kundi kubwa la kwenu itabidi tumalizie muwe wa mwisho.

Waheshimiwa Wabunge, katika hilo kundi kubwa tutapiga picha makundi manne na hayo makundi manne yatagawanyika kwa *zones* ama niseme kanda, lakini ninamaanisha mistari, hizi *rows* za viti hapa ndani. Kuanzia Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu hapa pamoja na *row* hii nyingine ya pili (hizi mbili) zitakuwa za kwanza (kundi la kwanza) na *rows* mbili zinazofuatia zitakuwa kundi la pili na *rows* pia hizi mbili hapa zitakuwa kundi la tatu na kisha kundi la nne tutamalizia na *rows* hizi hapa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wakati huo wote nitaomba tutaendelea kuketi tusubiri maelekezo ambapo Mpambe wa Bunge atakuwa akiwainua kwenda kupiga picha. Makundi ambayo yatatangulia ya viongozi wakuu wafuatao; picha ya kwanza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atapiga picha na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti

wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Jaji Mkuu. Hiyo itakuwa ni picha ya kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, picha ya pili itakuwa ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika. Ni picha ya viongozi watatu tu.

Waheshimiwa Wabunge, picha ya tatu ni ya viongozi wakuu wa Kitaifa; Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jaji Mkuu na Marais Wastaafu.

Waheshimiwa Wabunge, picha ya nne, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hii ni ndefu kidogo; Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jaji Mkuu, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mheshimiwa Spika wa *EALA,* Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Naibu Waziri Mkuu, Naibu Spika, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma na Katibu wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, picha kuanzia ya tano mpaka picha ya 13 zitakuwa ni picha ambazo kundi la viongozi ambao nimewataja kwenye picha ya nne wote watabaki watakuwa wameketi, lakini wataongezeka sasa viongozi wafuatao; viongozi wa kitaifa wastaafu wote. Hiyo itakuwa ni picha ya kundi la tano.

Kundi la sita Waheshimiwa Wabunge wa *EALA* na viongozi wa dini; picha ya saba, itakuwa viongozi wa vyombo vya ulinzi na usalama; picha ya nane, Tume ya Utumishi wa Bunge na Kamati ya Uongozi; picha ya tisa, Makatibu wa Bunge wastaafu; picha ya 10, Makatibu Mezani na *page boys* pamoja na *page girls*; picha ya 11, Menejimenti ya Utumishi wa Bunge, na picha ya kumi na mbili wawakilishi wa vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu na picha ambayo itamalizia makundi manne ni ninyi Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niwape taarifa kwamba Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ameshawasili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyotangaza atapata nafasi ya kuingia moja kwa moja ndani kwa msafara. Kuna mtu amehoji mbona Mpambe wa Bunge nilikuwa sisemi jina? Nitasema, watakapokuwa wanaingia rasmi wapambe, nitasema! Na kwenye picha pia nitasema *page boys* na *page girls*' pia Mpambe wa Bunge lazima atakuwepo kwenye picha hiyo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu toka nimeingia hapa kuna ukimya, Wabunge wanazungumza nikawa nadhani nitasikia *story* za kuagana, lakini sisikii naamini kwa sababu wote watarudi. *(Makofi)*

Miaka mitatu iliyopita Mheshimiwa Waziri Mkuu ukiwa umeketi hapo, nilisema nimepewa heshima ya kuongoza ratiba hii, nami naomba nirudi na nimerudi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wanasema nafasi yangu haina Wajumbe inawezekana wapo ambao hawaonekani, lakini wapo. *(Kicheko)*

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wageni walioko Ukumbini walikaa kwa utulivu wakimsubiri Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania)*

**NDG. PATSON SOBHA – MSHEREHESHAJI:** Wheshimiwa Wabunge, pamoja na wageni, naamini mmesubiri sana. Mheshimiwa Rais atawasili muda siyo mrefu na nitatangaza, lakini wakati huu ninaomba nitangaze, Waheshimiwa Wabunge wale ambao walikuwa wamekata tiketi za *SGR* kuondoka saa 12 jioni, saa 11?

Sawa, wote kuanzia saa 11.15 jioni mpaka hiyo saa 12.40 jioni, Mkurugenzi Mkuu wa *TRC* anatambua hilo, amesema hizo tiketi zipatikane. Kwa hiyo, itabidi nitaje namba yangu sasa mzitume na nimfikishie muda huu, halafu ana-*reschedule,* ili muende zaidi ya muda ule, kuanzia saa moja-naa. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** *MC* na *ATC* je?

**NDG. PATSON SOBHA – MSHEREHESHAJI:** Waheshimiwa Wabunge, ya *Air Tanzania* bado sijapata habari.

**MBUNGE FULANI:** Basi tafuta.

**NDG. PATSON SOBHA – MSHEREHESHAJI:** Naam, namba yangu...

**MBUNGE FULANI:** Shabiby? *(Kicheko/Makofi)*

**NDG. PATSON SOBHA – MSHEREHESHAJI:** Waheshimiwa Wabunge, Shabiby hawajaniambia, lakini naamini anaweza akaleta basi mpaka hapa likawasubiri.

Waheshimiwa Wabunge, namba yangu ni 0767414427. Ndiyo namba hiyo hiyo ya *WhatsApp*, ahsante sana.

**MBUNGE FULANI:** Rudia.

**NDG. PATSON SOBHA – MSHEREHESHAJI:** Ni 0767414427.

Waheshimiwa Wabunge, niilitangaza hilo na tunaliratibu kwa maana tunapokea hizo *WhatsApp messages* zenu za tiketi, lakini sasa wengi wananipigia kuniuliza tena, kwa hiyo, nashindwa sasa kumtumia mtu anayehusika. Kwa hiyo, naomba wote ambao mmetuma kwenye namba ile ya *WhatsApp* msubiri, ili kusudi niweze kuzituma. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Shabiby toa neno.

**MBUNGE FULANI:** Saa 24.

**NDG. PATSON SOBHA – MSHEREHESHAJI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tusikilizane kidogo. Nilitangaza habari za *SGR*, tunaendelea kufanyia kazi, lakini nimepewa ujumbe sasa pia kwamba wale wanaosafiri kwa *Air Tanzania* ndege itasubiri mmalize kumsikiliza Mheshimiwa Rais.

**MBUNGE FULANI:** *Super Baraka! Super Baraka!*

**MBUNGE FULANI:** Na wale wa Shabiby inakuwaje?

**MBUNGE FULANI:** Shabiby, Abood?

**MBUNGE FULANI:** Tunaoondoka na Shabiby saa ngapi?

**MBUNGE FULANI:** Na Isamilo.

**MBUNGE FULANI:** Wale wa *Bunda Bus* saa ngapi? Wa Zakaria Tarime, tunaomba tujue.

**MBUNGE FULANI:** *Easter line*.

**MBUNGE FULANI:** Na *Super Baraka* ya Mtwara.

**MBUNGE FULANI:** Na wa Zuberi Mwanza jamani!

**MBUNGE FULANI:** *SATCO* ya Bunda inaondoka saa 11.30.

**MBUNGE FULANI:** Boni fuatilia ya *Bunda Bus* saa ngapi.

**MBUNGE FULANI:** *Super Feo! Super Feo! Super Feo* Songea.

**NDG. PATSON SOBHA - MSHEREHESHAJI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba turejee kwenye viti vyetu na tuanze kusikiliza utaratibu.

Waheshimiwa Wabunge, msafara wa kwanza utatanguliwa na Mpambe wa Bunge - Ndugu Mohamed Msangi na kufuatiwa na Mwenyekiti wa Bunge - Mheshimiwa Najma Murtaza Giga; Mheshimiwa Alhaji Zuberi Ali Maulid - Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar; Mheshimiwa Joseph Ntakirutimana - Spika wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki na Makatibu Mezani watatu; Ndugu Monica Mwaga, Ndugu Pili Omari na Ndugu Emmanuel Mpanda. Wakiingia watakwenda moja kwa moja viti vilivyo kushoto kwa Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

*(Hapa Msafara wa Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar – Mheshimiwa Zuberi Ali Maulid na Spika wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki - Mheshimiwa Joseph Ntakirutimana Ukiongozwa*

*na Mwenyekiti wa Bunge Mheshimiwa Najma Murtaza Giga Uliingia Ukumbini)*

**NDG. PATSON SOBHA - MSHEREHESHAJI:** Waheshimiwa Wabunge, msafara wa pili utatanguliwa na Mpambe wa Bunge Silvanus Mkanza na kufuatiwa na viongozi wafuatao; Mwenyekiti wa Bunge - Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika akifuatiwa na Mheshimiwa George Mcheche Masaju - Jaji Mkuu wa Tanzania na Makatibu Mezani; Ndugu Michael Chikokoto, *ndc*, Ndugu Aziza Makwai na Ndugu Mkuta Masoli. Wakiingia watakwenda kuketi mkono wa kushoto wa Kiti cha Spika. *(Makofi)*

*(Hapa Msafara wa Jaji Mkuu wa Tanzania - Jaji George Mcheche Masaju Ukiongozwa na Mwenyekiti wa Bunge - Mheshimiwa Deodatus P. Mwanyika Uliingia Ukumbini)*

**NDG. PATSON SOBHA - MSHEREHESHAJI:** Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni.

Msafara wa tatu utatanguliwa na Mpambe wa Bunge - Ndugu Sabi Rutiginga na kufuatiwa na viongozi wafuatao; Mwenyekiti wa Bunge - Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama; Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar - Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla; na Makatibu Mezani watatu; Ndugu Yona Kirumbi, Ndugu Bakari Kishoma na Ndugu Zainab Issa. Msafara huu utaelekea upande wa kulia wa Kiti cha Spika. *(Makofi)*

*(Hapa Msafara wa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla Ukiongozwa na Mwenyekiti wa Bunge - Mheshimiwa Joseph K. Mhagama Uliingia Ukumbini)*

**NDG. PATSON SOBHA - MSHEREHESHAJI:** Waheshimiwa Wabunge, msafara wa nne utatanguliwa na Mpambe wa Bunge Ndugu Hamza Idrisa na kufuatiwa na viongozi wafuatao; Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu - Naibu Spika wa Bunge; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi - Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Makatibu Mezani Ndugu

Ruth Makungu, Ndugu Athumani Hussein, *ndc* na Ndugu Asia Minja. *(Makofi)*

*(Hapa Msafara wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi Ukiongozwa na Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa A. Zungu Uliingia Ukumbini)*

**NDG. PATSON SOBHA - MSHEREHESHAJI:** Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni!

Sasa msafara unaokuja ni msafara wa tano, unaotanguliwa na Mpambe wa Bunge, Ndugu Peter Magati, utafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson - Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani; akifuatia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Katibu wa Bunge - Ndugu Baraka Leonard na Makatibu Mezani wengine Ndugu Aziza Waziri Kheir na Ndugu Joshua Chamwela, *ndc*. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge kama mnakumbuka nilitangaza nikasema sasa msafara! Na nika-*pause* kidogo; lazima kuwe na dakika chache kidogo, msafara sasa unaingia! Na nilikuwa nadhani nimemaliza kazi kwa sababu ikija Siwa bado sijapewa hadhi ya kusimama hapa ikija Siwa ndiyo maana nikaondoka haraka; lakini kwa kweli bado nimeambiwa unapaswa kutangaza wakati, sasa mwenyewe anaingia. Kwa hiyo, nitasimama hapa mpaka atakapokuwa amefika nitatangaza.

Bila shaka wote ni mashahidi kwamba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amewasili na anapokelewa na gwaride la heshima na akishamaliza ataelekea ndani ya ukumbi na hapo ndipo shughuli sasa ile ya kusikiliza hotuba yake itakapoanza.

Waheshimiwa Wabunge, kama ulivyo utaratibu, Mheshimiwa Rais anakwenda kwenye Chumba Maalum cha Spika na watakaofuatia nyuma yao ni Katibu wa Bunge na Makatibu Mezani watajipanga sasa pamoja na Mpambe wa Bunge kwa ajili

ya kuingia ndani ya Ukumbi wa Bunge. Subiri dakika chache itakuwa hivyo muda si mrefu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa uvumilivu huu mlio nao ndiyo maana wananchi wanawataka tena.

**MBUNGE FULANI:** *MC* tunakupenda bure kwa siku ya leo.

**NDG. PATSON SOBHA – MSHEREHESHAJI:** Waheshimiwa Wabunge, msafara unaoongozwa na Mpambe wa Bunge, Peter Magati ukifuatiwa na Dkt. Tulia Ackson - Spika wa Bunge na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ndugu Baraka Lenard - Katibu wa Bunge; Makatibu Mezani Ndugu Aziza Waziri Kheir na Ndugu Joshua Chamwela, *ndc* sasa unaingia ukumbini. *(Makofi/Vigelegele)*

*(Hapa Msafara wa Spika wa Bunge Mhe. Dkt. Tulia Ackson na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Uliingia Ukumbini*

**SPIKA:** Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge na wageni wote, sasa tunaweza kuketi.

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunao viongozi wengi ambao wako hapa, wamealikwa na Bunge, nasi tunawashukuru sana kwa kuja kuungana nasi na wewe pia Mheshimiwa Rais tunakushukuru sana, sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, makofi haya ni kwamba Waheshimiwa Wabunge hawa pamoja na mambo mengine, wamefurahi kukuona, lakini hata usipokuwepo huwa wanapiga makofi mengi likitwajwa jina lako humu ndani, ahsanteni sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa wakati huu niwatambue wageni wote ambao walipata mwaliko wa Spika na wamepata fursa ya kuja kuungana nasi na tunawashukuru sana kwa kuja siku ya leo ya kihistoria kabisa ambayo Rais wetu

anakuja kuhitimisha Shughuli za Bunge la 12. Ahsanteni sana kwa kuja wageni wetu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, uniruhusu sasa niwatambulishe baadhi ya wageni hawa ambao leo tuko nao hapa ndani. Kwanza kabisa, nimtambue Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi ambaye amekuja kuungana nasi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa inabidi niwe nimemaliza kumtaja mgeni ndiyo tushangilie, kwa sababu vinginevyo jina moja litashangiliwa mara mbili/tatu hivi. Kwa hiyo, nimlete kwako Mheshimiwa Rais, Dkt. Hussein Ali Mwinyi ambaye ni Rais wa Zanzibar lakini pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Karibu sana na ahsanteni sana. *(Makofi/Vigeregere)*

Yupo pia Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah ambaye ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, yupo pia Mheshimiwa George Mcheche Masaju ambaye ni Jaji Mkuu wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, pia tumeungana na Mheshimiwa Zuberi Ali Maulid ambaye ni Spika wa Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Yupo pia Mheshimiwa Joseph Ntakarutimana ambaye ni Spika wa Bunge la Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, hawa ni wageni ambao wameruhusiwa kuingia katika Ukumbi huu wa Bunge. Sasa niwalete kwako wageni waliokaa majukwaa yetu ya wageni na tutawatangaza wageni waliokaa Jukwaa la Spika.

Kwanza, tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Awamu ya Nne wa Tanzania, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye ambaye ni Waziri Mkuu Mstaafu, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Yupo Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda ambaye ni Waziri Mkuu Mstaafu na Mzee wa Dodoma. *(Makofi)*

Yupo pia Mheshimiwa Anne Semamba Makinda ambaye ni Spika wa Bunge Mstaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, yupo pia Mheshimiwa Stephen Masato Wassira ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi ambaye ni Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi, ahsanteni sana, ahsanteni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Rais, pamoja na kwamba Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi ni Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi, lakini Bunge linamtambua pia kwamba ni Mgombea Mwenza wako kupitia Chama Cha Mapinduzi awe Makamu wa Rais. Ahsanteni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Yupo pia Ndugu John Mongela - Naibu Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi Tanzania Bara na Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Mohamed Said Mohamed ambaye ni Naibu Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi Zanzibar. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Rabia Abdallah Hamid ambaye ni Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi, Mambo ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Yupo pia *CPA* Amos Gabriel Makala ambaye ni Katibu wa Halmashauri Kuu wa Taifa ya Chama Cha Mapinduzi, Itikadi na Uenezi. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Mary Pius Chatanda ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi, ahsante sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Yupo pia Ndugu Adam Kimbisa, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Dodoma, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Mheshimiwa Rosemary Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Mheshimiwa Balozi Dkt. Moses Mpogole Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Mheshimiwa Mhandisi Zena Ahmed Said ambaye ni Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo Luteni Jenerali Salum Haji Othman, Mnadhimu Mkuu wa Majeshi akimwakilisha Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jocob John Mkunda, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Inspekta Jenerali Camilius Wambura ambaye ni Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Suleiman Abubakari Mombo ambaye ni Mkurugenzi Mkuu Idara ya Usalama wa Taifa, karibu sana. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Jeremiah Joram Katungu ambaye ni Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu John William Masunga ambaye ni Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. *(Makofi)*

Yupo pia Dkt. Anna Peter Makakala, Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Crispin Francis Chalamila ambaye ni Mkurugenzi Mkuu Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Haya ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Ahsanteni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wabunge, Ndugu Chalamila makofi hayo yanaashiria jambo lingine kabisa. Ahsanteni sana. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Ahsanteni sana na Wabunge wengine wanasema hawakufahamu, lakini watakufahamu muda siyo mrefu, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

Yupo Ndugu Aretas James Lyimo ambaye ni Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Dawa za Kulevya, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu James Kaji ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA),* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Dkt. Jim Yonazi ambaye ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Kaspar Mmuya, Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Yupo pia Mheshimiwa Jaji Francis Mutungi, Msajili wa Vyama vya Siasa, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Balozi Yusuph Mndolwa ambaye ni Mkuu wa Itifaki *(Chief of Protocol)*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Dkt. Thomas Kashililah, Katibu wa Bunge Mstaafu, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Stephen Kagaigai ambaye ni Katibu wa Bunge Mstaafu, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo pia Sheikh Abubakar Zubeir Ally, Sheikh Mkuu na Mufti wa Tanzania, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Dkt. Dickson Chilongani, Makamu Askofu Mkuu Kanisa la Anglikana Tanzania na Askofu wa *DCT,* karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Mchungaji Dkt. Magnus Mhiche ambaye ni Makamu Askofu Mkuu Makanisa ya *Pentecost (TAG)*. *(Makofi)*

Yupo Askofu Nelson Kisare ambaye ni Askofu Mkuu Kanisa la Mennonite na Mwenyekiti wa Kamati ya Viongozi wa Dini, karibu sana. *(Makofi)*

Pia yupo Musa Richard Mwacha ambaye ni Kiongozi wa Kanisa la *Fresh Spring Fellowship Church* Tanzania, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Mheshimiwa Haroon Pirmohamed, Mbunge Mstaafu wa Mbarali. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Pia yupo Dkt. Theodros Bekele Endialalu ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa *Suzan Buffet Fund,* karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao viongozi mbalimbali ambao pia wako nasi siku ya leo na mniruhusu niwatambue kwa makundi.

Sasa tunataka kuwatambua Makatibu Wakuu walio pamoja nasi. Wote wasimame kwa pamoja, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa na Washirika wa Maendeleo. Wote wasimame kwa pamoja na karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mheshimiwa Angela Kizigha, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo Wakuu wa Idara na Makatibu Wakuu wa Taifa wa Jumuiya za Chama Cha Mapinduzi. Wote wasimame kwa pamoja na karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo Wakuu wa Wilaya za Mkoa wa Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo Wakuu wa Mashirika ya Umma na Binafsi, Taasisi za Fedha na Taasisi za Elimu, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo Wakuu wa Taasisi za Vyombo vya Habari, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo Wawakilishi wa Vyama vya Siasa vyenye usajili wa kudumu, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia tunao Wawakilishi wa Asasi za Kiraia na Sekta Binafsi, karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, baada ya kuwatangaza wageni hawa, unayo picha sasa ya watu watakaokuwa wakikusikiliza hapa, lakini Taifa zima leo linasubiri kumsikiliza Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, sasa nitumie fursa hii kukukaribisha ili uje utoe hotuba yako ya kulifunga Bunge la 12.

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, karibu. *(Makofi)*

**HOTUBA YA KUHITIMISHA BUNGE LA KUMI NA MBILI**

**MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN - RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Frederick Sumaye na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, Mawaziri Wakuu Wastaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati; Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri; Waheshimiwa

Wenyeviti na Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Hamza Saidi Johari, Mwanasheria Mkuu; na Ndugu Baraka Leonard, Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; viongozi mbalimbali waalikwa wenzangu siku hii, mabibi na mabwana, habari za mchana.

**WOTE:** Nzuri.

**MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN - RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!

**WOTE:** Kazi Iendelee!

**MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN - RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mheshimiwa Spika, hakika tuna kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kufikia kushuhudia shughuli hii adhimu katika historia ya Bunge letu Tukufu. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inanitaka leo kuhutubia Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuhitimisha shughuli za Bunge hili, ili kuwezesha kuanza kwa mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa nafasi hii ya kulihutubia Bunge ili niweze kutimiza wajibu wangu huu wa msingi wa Kikatiba. Shukrani nyingi ni kwa uongozi wako shupavu, mahiri na wenye weledi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakika umeliongoza vyema Bunge hili na kukamilisha Mikutano 19 katika Bunge hili la 12. Ninajua haikuwa kazi rahisi, lakini pia ni kazi nyepesi kwako kwani kwenye wengi kuna mengi na kila mmoja na kichwa chake ndani ya Bunge hili, kwa hiyo, haikuwa kazi rahisi kwako. Ila kwa uhodari mkubwa umeweza kufikisha mashua yetu bandarini kama wanavyofanya manahodha makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika historia ya nchi yetu, wewe ni mwanamke wa pili kushika wadhifa huu wa juu kabisa katika

mhimili huu wa kutunga sheria. Hakika hujatuangusha wanawake wenzio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uzoefu wako wa kitaifa na kimataifa umekuwa chachu inayohakikisha kazi hii inafanyika kwa viwango vya hali ya juu na hivyo kuendelea kulijengea heshima Bunge letu. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nikupongeze kwa kutekeleza majukumu haya sambamba na majukumu yako ya Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani. Kule nako umeweka historia ya kuwa mwanamke wa kwanza kutoka Afrika kuchaguliwa kushika nafasi hiyo. Tunakupongeza sana kwa kuitumikia ipasavyo nafasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile niwashukuru Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kutekeleza majukumu yao kwa uzalendo na kwa weledi, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halikadhalika, nitoe shukrani na pongezi zangu za dhati kwenu ninyi Waheshimiwa Wabunge kwa kazi kubwa na nzuri mliyoifanya. Mmetimiza ipasavyo wajibu wenu wa kuwawakilisha wananchi, kutunga sheria na kusimamia Serikali. Bunge hili limekuwa na mchango mkubwa katika kuleta maendeleo na ustawi wa wananchi. Bila shaka ninyi wawakilishi wa wananchi mmeielewa vyema dhana ya maendeleo ya watu, kwamba hatua na jitihada zote za Serikali hazina budi kuelekezwa kwenye kuboresha maisha ya kila Mtanzania. Hili limesaidia kujijengea ninyi wenyewe Wabunge heshima kubwa, lakini pia heshima ya Bunge letu kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina budi kutambua mchango na mafanikio ya Waheshimiwa Wabunge waliotuwakilisha kwenye majukwaa ya Mabunge ya Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na Jumuiya ya Ukanda wa Maziwa Makuu. Kipekee, nimpongeze Dkt. Deo Mwapinga kwa kuchaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa Jukwaa la Mabunge ya Jumuiya ya Ukanda wa Maziwa Makuu. Ni wazi

kuwa mmeitendea haki demokrasia ya Tanzania na kuliletea heshima kubwa Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nitumie fursa hii kulishukuru tena Bunge hili kwa tuzo mliyonipatia kwa kutambua na kuthamini...*(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, ninawashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua na kuthamini mchango wangu katika maendeleo na ustawi wa nchi yetu. Ila kama nilivyosema siku nikipokea tuzo hiyo, mafanikio haya yaliyopatikana yanatokana na mchango mkubwa wa Bunge, viongozi wenzangu Serikalini, pamoja na Watanzania wote. Kwa hiyo, tuzo ile ni yetu sote. Ninawashukuru sana kwa ushirikiano wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru watangulizi wangu ambao leo hii nipo nao hapa. Kwa kuwa nilisimama juu ya mabega yao na kuweza kujifunza, hakika misingi imara waliyoiweka imewezesha kupatikana kwa mafanikio haya mbalimbali katika kipindi changu cha miaka minne.

Mheshimiwa Spika, nikiri tu kwamba misingi yao na ushauri wao kwa wale niliobahatika kufanya kazi nao, umenisaidia sana mimi binafsi pamoja na Serikali ninayoiongoza. Nimefurahi kuona Mheshimiwa Rais Mstaafu Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete yuko hapa pamoja na Makamu wa Rais Wastaafu; na pia Mawaziri Wakuu Wastaafu, tuko nao hapa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuwashukuru sana viongozi hawa kwa msaada wa kimawazo na ushauri ambao wameendelea kunipa katika kipindi chote cha uongozi wangu. Hakika nimeamini kuwa wazee ni dawa na palipo na wazee hapaharibiki jambo. Ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikimalizia shukrani zangu ila siyo kwa umuhimu, niwashukuru waajiri wangu Watanzania. Hakika wao ndiyo hamasa na chachu ya mimi kufanya yote haya.

Ninawashukuru kwa sala, dua na maombi yao, bila kusahau ushirikiano mkubwa wa hali na mali katika kulijenga Taifa au kuijenga Tanzania tunayoitaka na Taifa linalotumainiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu Bunge hili la 12 lianze kuna viongozi, ndugu jamaa na marafiki waliotutoka. Kama tunavyojua tuliondokewa na Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano; vilevile tuliondokewa pia na Hayati Mzee Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili; Hayati Cleopa David Msuya, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu; na Hayati Edward Ngoyai Lowassa aliyewahi kuwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, hata katika Bunge hili wako pia Wabunge wenzetu tulikuwa nao wakati nikizindua Bunge hili tarehe 22 Aprili, 2021, ila sasa wametangulia mbele ya haki. Tutaendelea kuwakumbuka Mheshimiwa Martha Umbulla - Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Atashasta Nditiye - Mbunge wa Jimbo la Muhambwe; Mheshimiwa Khatib Haji - Mbunge wa Jimbo la Konde; Mheshimiwa Elias Kwandikwa - Mbunge wa Jimbo la Ushetu; Mheshimiwa William Ole Nasha - Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro; Mheshimiwa Irene Ndyamkama - Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Mussa Mussa - Mbunge wa Jimbo la Amani; Mheshimiwa Francis Mtega - Mbunge wa Jimbo la Mbarali; na Mheshimiwa Ahmed Abdulwakil - Mbunge wa Jimbo la Kwahani; na vilevile Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile - Mbunge wa Jimbo la Kigamboni. Hivyo, ninaomba tusimame kwa dakika moja kuwaombea, Mwenyezi Mungu azipumzishe roho zao mahali pema peponi.

*(Hapa Wabunge na Wageni Waalikwa Walisimama Kuwaombea Waliotangulia Mbele ya Haki)*

**MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN - RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** *Amin*.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kuwa tarehe 22 Aprili, 2021 takribani mwezi mmoja baada ya kushika wadhifa wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nilihutubia Bunge hili. Nilieleza

mtazamo wangu kuhusu nchi yetu na kutaja vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Sita. Vilevile, vipaumbele vilivyobainishwa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 – 2025. Niliahidi kudumisha mema ya awamu zilizopita, kuendeleza mema yaliyopo na kuleta mema mapya. Pia niliahidi kufanya mabadiliko pale itakapobidi kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo ada, tunapohitimisha shughuli za Bunge, ninaomba kutumia fursa hii sasa kutoa mrejesho wa utekelezaji wa majukumu ya Serikali na yale ambayo tuliahidi kufanya. Ninapenda kusema, maendeleo ni hatua, na tumesikia kutoka kwa Mawaziri mbalimbali pamoja na Wabunge kazi iliyofanywa na Serikali. Hata hivyo, kwa kuwa mimi ndiye niliyetoa ahadi mbele ya Bunge hili, ninawajibika kutoa mrejesho hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ninafurahi kusema kuwa kipindi hiki kimekuwa ni cha kufanya mageuzi makubwa, kuongeza tija kwenye shughuli za kiuchumi na kujenga msingi imara wa ukuaji endelevu wa kiuchumi wenye kasi zaidi na unaowainua watu kiuchumi. Vilevile, kimekuwa ni kipindi cha kuimarisha ustahimilivu wa jamii, kukuza ustawi wa wananchi na kuwawezesha kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nilipokabidhiwa dhamana ya kuiongoza nchi yetu, niliahidi kudumisha tunu za Taifa letu (amani, umoja na mshikamano), uhuru wa nchi yetu, Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar pamoja na kudumisha Muungano wetu. Kama ilivyokuwa kwa Serikali za Awamu zilizopita, tumeshuhudia nchi yetu ikiendelea kujivunia tunu hizo na kuziimarisha. Nyote ni mashahidi wa namna nchi yetu Tanzania imeendelea kuwa nchi moja na Watanzania wanaendelea kuwa wamoja wenye ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania wameendelea kuwa wamoja wenye mashirikiano licha ya kuwa na tofauti zao za kidini, mila na desturi, itikadi za kisiasa na hata ushabiki wa michezo (Simba na Yanga). Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninatambua Namungo pia na ninatambua *Singida United*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtakumbuka kuwa katika hotuba yangu ya kufungua Bunge nilisisitiza umuhimu wa viongozi wa pande zote mbili za Muungano kukutana na kuzungumzia ustawi wa Muungano wetu. Ninafurahi kuwataarifu kwamba maagizo yangu yale yametekelezwa kwa ufanisi zaidi chini ya Uenyekiti wa Makamu wa Rais akisaidiwa na Waziri Mkuu kwa upande wa Tanzania Bara na kwa upande wa Zanzibar Makamu wa Pili wa Rais.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki tumepiga hatua kubwa hususan kwa kuzipatia ufumbuzi jumla ya hoja 15 za Muungano, hatua inayozidi kuongeza imani ya Watanzania kwa Serikali. Pamoja na hayo, niwaase Watanzania wenzangu tuendelee kushikamana na kuwa makini na vitisho vyovyote dhidi ya Muungano wetu. Pia niwasihi kuendeleza umoja, utulivu na amani vitu ambavyo ni sifa njema kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu iko salama, mipaka yetu ipo salama na imara kwa sababu Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kutimiza ipasavyo jukumu lake la kulinda uhuru na mipaka ya nchi yetu. Jeshi letu la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, lilitimiza miaka 60 tangu kuanzishwa kwake. Katika kipindi hiki tumewekeza sana katika kuliimarisha kwa vifaa, zana za kisasa na mafunzo. Weledi na nidhamu ya wanajeshi wetu ni ya hali ya kupigiwa mfano.

Mheshimiwa Spika, tumeboresha maslahi na makazi ya wanajeshi kwa kujenga nyumba mpya 6,064 za kuishi askari. Uwezeshaji huo umechangia kulifanya Jeshi letu kushiriki ipasavyo katika shughuli mbalimbali za kitaifa na kimataifa, ikiwemo ulinzi wa rasilimali, ulinzi wa miradi mikubwa ya kimkakati na *operation* za ulinzi wa amani za Umoja wa Mataifa, hasa nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Lebanon, Sudan au Sudan Kusini na eneo la Abyei.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), tumepanua miundombinu na kuongeza idadi ya vijana wanaojiunga na jeshi kutoka 160,427 mwaka 2020 hadi 190,059 mwaka 2025. Tumefanya hivyo kwa kutambua kuwa Jeshi la

Kujenga Taifa ni nyenzo muhimu ya kujenga ujasiri, uzalendo na dhana ya kujitegemea miongoni mwa vijana. Vilevile SUMA-JKT imeweza kushiriki kikamilifu kufanikisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya uzalishaji na miradi ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jeshi la Polisi, tumeendelea kuliimarisha kwa kuboresha mazingira ya kazi na kuongeza miundombinu ambapo vituo vya polisi 472 vimejengwa hadi ngazi ya kata na shehia. Halikadhalika, tumeboresha makazi ya askari na kununua vitendea kazi, ikiwemo magari na pikipiki, kwa ajili ya kazi za utawala na *operation.* Aidha, askari wapya 16,000 wameajiriwa, huku maofisa, wakaguzi na askari 10,363 wakipandishwa vyeo.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi nyingi kwa Jeshi la Polisi kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya. Hatuna budi kutambua kwamba uhalifu unaozuiliwa kwa jitihada za Jeshi la Polisi ni mkubwa kuliko unaofanyika. Kasi ya kuwabaini, kuwakamata wahalifu na kuwafikisha mahakamani imeongezeka. Jambo ambalo bado hatujafanikiwa vya kutosha ni ajali za barabarani; lazima nazo tuendelee kuzitafutia muarobaini wake. Aidha, nalielekeza Jeshi la Polisi kuongeza jitihada katika kukomesha matukio ya watu kupotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi letu la Magereza nalo limeendelea kutekeleza vizuri majukumu yake ya kulinda wafungwa na kurekebisha tabia zao. Aidha, katika kulinda haki za binadamu, tumeendelea kuboresha huduma za malazi, mavazi na chakula kwa wafungwa jinsi hali ya uchumi inavyoimarika. Kwa upande wa watumishi, Serikali imewapandisha vyeo maafisa waandamizi na askari wa jeshi hilo wapatao 14,733 na kuajiri askari wapya 3,404 hivyo kupunguza uhaba wa rasilimali watu.

Mheshimiwa Spika, vilevile tumewapa vitendea kazi ikiwemo magari, kwa ajili ya kuimarisha utendaji kazi. Magereza mpya nane pamoja na Hospitali Kuu ya Kanda ya Jeshi la Magereza Dodoma inaendelea kujengwa. Serikali imewezesha jumla ya magereza 66 kuanza kutumia mfumo wa TEHAMA wa Mahakama

Mtandao ambao unarahisisha usikilizaji wa kesi bila wafungwa kusafirishwa hadi mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza uwezo wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kufikia maeneo ya dharura kwa wakati, Serikali imewezesha ujenzi wa vituo vipya vya zimamoto; vitatu vilivyokamilika na vinane vinaendelea na ujenzi. Vilevile, vituo vya zamani vimefanyiwa ukarabati na kununua magari 12 ya kuzima moto, yakiwemo magari mawili yenye ngazi kwa ajili ya kufikia majengo marefu na boti mbili za uokoaji katika bahari na Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Idara ya Uhamiaji, zaidi ya maafisa, wakaguzi na askari 3,115 wamepandishwa vyeo na askari wapya 2,251 wameajiriwa. Aidha, doria, misako na *operation* zimeimarishwa katika maeneo mbalimbali nchini na kuwezesha kukamatwa watu 97,538 kwa makosa ya uhamiaji, ambao wamechukuliwa hatua za kisheria, ikiwemo kwa baadhi yao kuondoshwa nchini. Vilevile, tunaendelea na ujenzi wa Chuo cha Mafunzo cha Uhamiaji cha Raphael Kubaga kilichopo Boma Kichakamiba, Wilaya ya Mkinga, Mkoani Tanga.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeimarisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya kwa kupunguza uingizaji, uzalishaji na usambazaji wa dawa za kulevya kwa kubaini na kudhoofisha mitandao ya wafanyabiashara wa dawa za kulevya. Katika kipindi hiki tumekamata jumla ya kilogramu 4,697,511.35 za dawa za kulevya zikihusisha watuhumiwa 25,715. Kwa upande mwingine, katika kuwasaidia waathirika, tumeongeza vituo vya utoaji huduma za tiba kwa warahibu wa dawa za kulevya kutoka vituo tisa mwaka 2020 hadi 18 mwaka 2025, ili kupanua wigo wa huduma hii muhimu. Pamoja na hatua hizo, hatua nyingine madhubuti za kudhibiti na kuwalinda vijana wetu dhidi ya dawa hizo zinaendelea kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha mfumo wa usimamizi wa maafa, tumerekebisha Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Maafa ya mwaka 2004, Toleo la mwaka 2025 na tumetunga Sheria ya Usimamizi wa Maafa Na. 6 ya mwaka 2022 kwa lengo la kuweka

mfumo wa kitaasisi wa usimamizi wa maafa kuanzia ngazi ya Taifa hadi Wilaya. Nyote ni mashahidi wa maafa makubwa yaliyotufika kwa nyakati tofauti, kutokana na mvua kubwa kwenye maeneo ya Hanang, Mbeya, Rufiji na Moshi. Kipekee, navipongeza vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuwa mstari wa mbele na kushiriki katika uokoaji wakati wa maafa na vilevile usambazaji wa mahitaji muhimu kwa waathirika.

Mheshimiwa Spika, kufuatia maafa ya Hanang, Serikali iliratibu ujenzi wa nyumba 109 za kudumu zenye thamani ya shilingi bilioni 3.08 kwa ajili ya waathirika 745 ambao nyumba zao ziliharibiwa. Pia natambua mchango wa taasisi za kiraia, wafanyabiashara na wananchi waliojitolea na kushiriki kikamilifu katika mazoezi ya uokoaji, kama tulivyoona kwenye ajali ya ndege ya Bukoba, maporomoko ya Hanang na kuanguka kwa jengo Kariakoo. Huu ndio Utanzania na ninawapongeza tena kwa moyo wao wa utu na uzalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipoingia madarakani niliona haja ya kuhakikisha tunaendelea kujenga Taifa lenye maelewano na maridhiano ili tuweze kwenda pamoja katika muelekeo wa maendeleo. Dhima hii ilinisukuma kubuni na kutekeleza falsafa ya "R" nne. Tukiongozwa na falsafa hiyo, imetuelekeza kwenye mageuzi, maridhiano, ustahimilivu na kujenga upya. Tumeweza kuwaleta wadau wa kisiasa na wengineo pamoja na kufanya maamuzi na maboresho mbalimbali yaliyojumuisha na kushirikisha wadau wote. Serikali iliunda Tume ya Maridhiano iliyofanya kazi nzuri na ilikuja na mapendekezo ya aina mbili, yale ambayo ni ya muda mrefu, kama mabadiliko ya Katiba na yale ya muda mfupi, ambayo yalihusu masuala ya uhuru wa vyombo vya habari, vyama vya siasa kufanya shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mapendekezo ya Tume, Serikali iliondoa mara moja zuio la mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa na wote tumeshuhudia vyama vikiendelea kufanya shughuli zao kwa uhuru, ikiwemo mikutano ya hadhara kote nchini. Vilevile, Baraza la Vyama vya Siasa limefanya mikutano sita na kutoa mawazo na ushauri uliowasilishwa Serikalini na kufanyiwa kazi. Kufuatia mashauriano yaliyowahusisha wadau

wote wa kisiasa, Bunge limetunga Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 1 ya mwaka 2024, Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 2 ya mwaka 2024, Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258 na Sheria ya Gharama za Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi imeundwa kwa sheria yake yenyewe. Tumefanya ili kujibu rai ya muda mrefu ya wadau wa kisiasa nchini. Miongoni mwa maboresho kwenye Sheria ya Uchaguzi ni kuongeza takwa la kila mgombea kupigiwa kura hata akiwa mgombea pekee, hatua ambayo inafuta kilichojulikana kama mgombea kupita bila kupingwa. Vilevile, utungaji wa kanuni za uendeshaji wa uchaguzi umefanyika na Serikali imeendelea kuimarisha uendeshaji wa shughuli za vyama vya siasa nchini ambapo hadi Juni, 2025 Serikali imetoa ruzuku ya shilingi bilioni 87.87 kwa vyama vinavyostahili kupata ruzuku.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine asasi za kiraia nazo zimekuwa huru kufanya shughuli zao ikiwa ni pamoja na kukutana na kuishawishi Serikali ambapo mapendekezo yao mengi yamepokelewa na kufanyiwa kazi. Kwa kuwa suala la Katiba ni pendekezo la muda mrefu la Tume ya Maridhiano, kwa msingi huo, mchakato wa Katiba Mpya ni miongoni mwa ahadi ambazo zinaonekana katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2025-2030. Hivyo, ni kusema kuwa mchakato wa Katiba Mpya utatekelezwa katika kipindi kijacho cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa rushwa ni adui wa haki, na mlifurahi sana mlipomuona Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa na hatanii sasa kwa kuwa rushwa ni adui wa haki na ni kikwazo kwa maendeleo, Serikali imeongeza nguvu kwenye mapambano dhidi ya rushwa. Jitihada hizo zimeiwezesha Tanzania kushika nafasi ya pili katika Ukanda wa Afrika Mashariki na nafasi ya 14 kwa nchi za Afrika kwenye mapambano dhidi ya rushwa. Hii ni kwa mujibu wa taarifa ya Taasisi ya *Transparency International* ya mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki tumedhibiti na kuokoa kiasi cha shilingi bilioni 211.95 na kuzirejesha Serikalini kupitia

*operation* mbalimbali za uchunguzi wa tuhuma za rushwa. Aidha, mali zenye thamani ya shilingi bilioni 35.688 zikijumuisha nyumba, viwanja, magari na fedha taslimu shilingi bilioni 1.17 zilitaifishwa. Katika jitihada hizi natoa rai kwa Watanzania kuendelea kutoa ushirikiano katika mapambano dhidi ya rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutimiza ipasavyo wajibu wake kwa mhimili wa dola wa kutunga sheria. Katika kipindi cha uhai wa Bunge la 12 kumepitishwa miswada 60, maazimio 922 na vilevile Serikali imetoa taarifa 15 kupitia kauli za Waheshimiwa Mawaziri Bungeni kwa ajili ya kutoa ufafanuzi wa masuala yenye maslahi mapana kwa Taifa. Hakika mmefanya kazi kubwa kwani michango na ushauri wa Bunge hili umekuwa chachu kwa baadhi ya hatua tulizochukua kwenye mabadiliko ya kisera, kisheria na kiutendaji yaliyofanywa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeongeza kiwango cha Mfuko wa Jimbo kutoka shilingi bilioni 11 mwaka 2021/2022 hadi shilingi bilioni 15.9 kuanzia mwaka 2022/2023 hadi sasa ili kurahisisha utendaji wenu majimboni na kuchochea maendeleo. Ni matumaini yangu kwamba fedha hizi mlizitumia vyema katika kuwaletea wananchi maendeleo, vinginevyo wakati ni sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Uchaguzi Mkuu ndio mazungumzo makubwa nchini kwa sasa. Nasema kuwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi itatangaza hivi karibu tarehe ya siku ya uchaguzi. Zoezi la uandikishwaji limeisha nchi nzima. Zoezi la kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura limekamilika kwa awamu mbili kama ambavyo sheria inaelekeza. Sote tumeshuhudia mwitikio mzuri wa wananchi kujitokeza kwenye vituo vya kuandikisha wapiga kura na ninawapongeza wananchi wote kwa kujitokeza kwao. Tunatarajia kwamba tume itatutangazia idadi ya wapiga kura.

Mheshimiwa Spika, uhuru wa habari; mtakubaliana nami kuwa uhuru wa habari na uhuru wa watu kutoa maoni yao umeongezeka, majukwaa ya kutolea habari nayo yameongezeka tofauti na hapo awali. Sasa hivi kutokana na kukua kwa matumizi ya mtandao na kuongezeka kwa majukwaa

ya kidijitali habari nyingi zinapatikana kiganjani. Serikali imetoa leseni kwa magazeti na majarida 356, vituo vya redio 247, vituo vya televisheni 68, redio na televisheni za mitandaoni 325 na *blogs* 72.

Mheshimiwa Spika, tuna magazeti ya kila siku na kamwe Serikali haijafanya uhakiki wa habari kabla hazijachapishwa au kuandikwa. Tunafanya hivi tukiamini waandaaji wa maudhui haya ni watu wenye weledi wa kutosha na kwamba tunafahamu ustawi wa demokrasia yetu unategemea sana uhuru wa vyombo vyetu vya habari. Tunathamini na kutambua mchango mkubwa wa vyombo vya habari katika kuelimisha jamii, kupambana na maovu pamoja na kuhimiza uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, katika kulinda na kutambua mchango wa waandishi wa habari kwa jamii tumefanya marekebisho ya Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 na kanuni zake. Pia tumeandaa *Tuzo za Samia Kalamu Awards* kutambua waandishi wa habari za maendeleo Tanzania. Pamoja na hatua zote hizi hatukusita wala kuchelea kuchukua hatua pale uhuru huu ulipotumiwa vibaya na kutishia kuleta vurugu nchini pamoja na kuvuruga usalama wa jamii au pale uhuru huu umekiuka sheria za nchi au maadili, mila na desturi za Kitanzania. Hivyo basi tutaendelea kusimamia uhuru wa vyombo vya habari wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ya uchumi Tanzania; Serikali imeendelea kuelekeza nguvu kwenye sera za uchumi jumla na sera za uchumi katika ngazi ya chini zinazogusa wananchi wa kawaida. Ni wazi kuwa kazi hii haikuwa nyepesi wala rahisi kutokana na hali ya UVIKO-19 na migogoro ya kikanda inayoendelea ambayo imesababisha uchumi wa duniani kutetereka. Ili kukabiliana na hali hii Serikali ilichukua hatua mbalimbali za kisera, kiutawala na uwekezaji ili kukuza uchumi wa nchi yetu. Ni wazi kuwa jitihada zetu zilizaa matunda, ukuaji wa uchumi wa nchi ulipanda kutoka wastani wa 3.9% mwaka 2021 hadi 5.5% mwaka 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukuaji huu uko juu ya wastani wa ukuaji wa Bara la Afrika ambao ni 4% kwa mwaka 2024. Aidha, wakati uchumi wa dunia unatarajiwa kukua kwa wastani wa 2.3% mwaka 2025, Shirika la Fedha Duniani linakadiria kuwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa Tanzania mwaka huu wa 2025 utafikia 6%. Pato ghafi la Taifa limeongezeka kutoka shilingi trilioni 156.4 mwaka 2021 hadi kufikia shilingi trilioni 205.84 mwaka 2024. Hivyo basi, pato la wastani la Mtanzania nalo limeongezeka kutoka shilingi 2,397,411 mwaka 2020 hadi shilingi 2,938,634 mwaka 2024. Pia shilingi yetu imeendelea kuimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiashiria kingine muhimu cha utulivu wa uchumi ni mfumuko wa bei ambao uliendelea kuwa chini ya 5% kwa miaka yote minne. Kiwango hiki si tu kipo ndani ya lengo letu kama nchi la kuhakikisha hakizidi 5% bali pia ni miongoni mwa viwango bora Afrika Mashariki na kiko chini ya wastani wa mfumuko wa bei ulioshuhudiwa Barani Afrika. Hali hii inatokana na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti na uhakika wa upatikanaji wa chakula katika masoko ya ndani kutokana na kukuza tija katika kuzalisha au uzalishaji wa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mauzo yetu ya bidhaa nje ya nchi yameongezeka kutoka dola za Marekani bilioni 6.39 mwaka 2021 hadi kufikia dola za Marekani bilioni 8.7 mwaka 2024 na kutunisha akiba yetu ya fedha za kigeni ambapo hadi mwezi Aprili, 2025 tulikuwa na akiba ya dola za Marekani bilioni 5.6 inayotosheleza kuagiza bidhaa na huduma kwa miezi nne na nusu, kama lilivyo lengo la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, kufuatia marekebisho ya Sheria ya Madini, Sura ya 123, Benki Kuu ya Tanzania iliweza kununua na kuweka na kuwa na akiba ya kilo za dhahabu 3,424 zilizonunuliwa kwa gharama ya shilingi bilioni 702.3. Ununuzi unaendelea ili kuimarisha zaidi kiwango cha akiba tulichonacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la makusanyo ya kodi; nililielezea Bunge kwamba ningependa kuona wafanyabiashara, wawekezaji na wananchi wanaelimishwa na kutambua kwamba kodi ndio msingi wa maendeleo ya nchi na hivyo wawezeshwe kulipa kodi bila kutumia mabavu. Katika kufikia azma hii, Serikali

imeimarisha mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji mapato, udhibiti wa mianya ya kupoteza mapato, kuanzisha Jukwaa la Kodi na Uwekezaji na kuijengea uwezo Mamlaka ya Mapato Tanzania na mamlaka nyingine za ukusanyaji mapato ya Serikali. Jitihada hizo zimeongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa mwezi kutoka shilingi trilioni 1.51 mwezi Novemba, 2020 hadi shilingi trilioni 3.09 mwezi Machi. *(Makofi)*

Ninashukuru, Waheshimiwa Wabunge.

Kwa hiyo, tumefikia shilingi trilioni 3.09 mwezi Machi mwaka huu 2025, ikiwa ni ongezeko la 104%. Ili kuimarisha zaidi usimamizi wa kodi nchini, niliunda Tume ya Rais ya Marekebisho ya Kodi ambayo tunatarajia itakuja na mapendekezo yatakayoleta mageuzi ya kiutendaji kwenye mifumo ya utozaji na ukusanyaji wa kodi nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kutoa huduma bora kwa wananchi, bajeti ya Serikali imeongezwa kutoka shilingi trilioni 34.88 mwaka 2020/2021 hadi shilingi trilioni 50.29 mwaka 2024/2025, ikiwa ni ongezeko la wastani wa 8.84% kwa mwaka. Ninalishukuru sana Bunge hili kwa kupitisha bajeti hizo. *(Makofi)*

Kwa kweli, bajeti zilizokuwa zikipitishwa na Bunge hili zimekuwa kichocheo kikubwa cha maendeleo kwa kuboresha huduma za kijamii na kuwezesha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Mei, 2025 deni la Serikali lilifikia shilingi trilioni 107.7. Kati ya deni hilo, deni la nje ni shilingi trilioni 72.94 na deni la ndani ni shilingi trilioni 34.76. Kuongezeka kwa deni la Serikali kumetokana na sababu mbalimbali. Mojawapo ni kupokelewa kwa fedha za mikopo mipya na ya zamani ambayo mikataba yake iliingiwa tangu Serikali za awamu ya nyuma kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ni vyema tukafahamu kuwa mkopo unaweza ukasainiwa leo, lakini fedha husika zikaanza kupokelewa baada ya maandalizi ya mradi kukamilika na mradi kuanza. Hivyo, ili liwe deni au mkopo huo uingie kwenye deni la Serikali ni lazima Serikali iwe imepokea

fedha hizo, huduma au vifaa tulivyokubaliana. Hivyo, ni vyema wananchi wakaelewa kuwa katika Awamu ya Sita, pamoja na kusaini mikopo mipya, lakini pia tunaendelea kupokea fedha za mikopo ambayo ilisainiwa katika vipindi tofauti na kuongeza kiasi cha deni la Serikali. Kwa mfano, Awamu ya Sita imepokea kiasi cha shilingi trilioni 11.3 ikiwa ni mikopo iliyosainiwa na awamu zilizopita.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine ya ongezeko la deni la nje ni kuimarika kwa dola ya Marekani dhidi ya shilingi ya Tanzania. Kwa mfano mwezi Machi, 2021 kiwango cha kubadilisha shilingi ya Tanzania dhidi ya dola za Marekani kilikuwa shilingi 2,298.5 wakati Machi, mwaka huu 2025 kiwango hicho kilikuwa 2,650. Hivyo, endapo deni la Serikali litatajwa kwa shilingi za Tanzania ni lazima lionekane limeongezeka. Mathalani kwa sasa deni limeongezeka kwa zaidi ya shilingi trilioni 3.9 kutoka na *exchange rate*. Hatua hii ya kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani isichukuliwe kama ni hatua hasi bali ilikuwa ni hatua muhimu ya kukabiliana na mtikisiko wa uchumi wa dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mwenendo wa ulipaji wa deni la Serikali, ninapenda kutaarifu kuwa malipo ya deni la Serikali yamekua yakiongezeka kutoka shilingi trilioni 8.22 mwaka wa fedha 2020/2021 hadi kufikia makadirio ya shilingi trilioni 14.20 kwa mwaka 2025/2026. Ongezeko hili ni kutokana na kuiva kwa mikopo ya muda mrefu na mikopo yenye masharti ya kibiashara iliyokopwa katika awamu zilizopita kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Aidha, kuongezeka kwa malipo ya deni hasa la nje kumesababishwa pia na mabadiliko ya mara kwa mara ya riba katika masoko ya fedha ya kimataifa kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo athari za UVIKO-19 na uamuzi wa Hazina ya Marekani kubadilisha viwango vya riba vya dhamana za Serikali ya nchi hiyo. Mabadiliko hayo yalisababisha baadhi ya nchi zinazoendelea hasa Afrika kushindwa kulipa madeni kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ongezeko la deni la Serikali la ndani limechangiwa na mikopo ya kugharamia miradi ya maendeleo na kulipa madeni ya ndani yaliyoiva kwa wawekezaji wa dhamana za Serikali kwa utaratibu wa kulipia mtaji wa dhamana za Serikali zilizoiva. Aidha, tulifanya maamuzi ya kutambua madeni mengine ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa Serikali kupitia hati fungani maalum isiyo taslim yenye thamani ya shilingi trilioni 2.67. Kati ya kiasi hicho shilingi trilioni 2.18 ni madeni ya *PSSSF* ya waliokuwa wafanyakazi wa Serikali kabla ya 1999 (maarufu kama *pre-99);* shilingi bilioni 433.71 ni madeni ya *NSSF* ya muda mrefu; na shilingi bilioni 63.52 ni madeni ya Kampuni ya Ubia ya Mifuko ya *Pension* yaani *PPP (Pension Property Limited*).

Mheshimiwa Spika, kampuni hii ilifadhili miradi ya Serikali kwa kutoa mikopo kwa vipindi tofauti kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya Serikali ambayo ni ujenzi wa ukumbi wa Bunge-Dodoma na ujenzi wa Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela, Arusha. Madeni haya hayakuwahi kuwa sehemu ya deni la Serikali. Kiasi cha shilingi trilioni 2.2 kilichobaki kinatarajiwa kuanza kutambuliwa ndani ya miaka mitatu ijayo kwa kuanzia na mwaka wa 2025/2026; ambapo deni la kabla ya mwaka 1999 kiasi cha bilioni 630 litatambuliwa na deni la *NHIF* kiasi cha bilioni 180 zilizotumika kujenga Hospitali ya Benjamin Mkapa, Dodoma.

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hizi ni kunusuru mifuko ya hifadhi ya jamii yenyewe, lakini pia kuhakikisha kuwa wastaafu wetu waliolitumikia Taifa wanapata mafao yao kwa wakati. Kwa ujumla, tumeyatambua madeni haya na kuyaweka kwenye deni la ndani la Serikali ili kutoa nafuu kwa mifuko yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona niyaseme haya kwa urefu ili Watanzania waelewe kuhusu suala hili la deni la Taifa ambalo hupotoshwa mara kwa mara. Aidha, niwahakikishie Watanzania kuwa Serikali inaendelea kuchukua hatua kuhakikisha deni linaendelea kuwa himilivu. Tutaendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi wa mikopo katika ugharamiaji wa bajeti zetu. Tutaendelea kuelekeza fedha za mikopo katika miradi inayokuza mapato ya ndani na mauzo ya

bidhaa na huduma nje ya nchi. Tutaendelea kuhakikisha kuwa maafisa masuuli wanazingatia maandalizi ya msingi ya mradi kabla ya kuingia mikataba kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo ikiwemo Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada Sura 134. Vilevile, tutaendelea kuimarisha ufuatiliaji na usimamizi wa miradi inayotekelezwa kwa mikopo ili kuhakikisha kuwa inaleta tija iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa nidhamu ya matumizi ya fedha na mali za Serikali tumeendelea kuelekeza nguvu zetu katika kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, kuimarisha utaratibu wa manunuzi Serikalini na ukaguzi wa hesabu za Serikali. Kwa upande wa ununuzi wa bidhaa na huduma, tumehakikisha kuwa Sheria ya Mamlaka ya Ununuzi wa Umma inafanya kazi ipasavyo ili kuhakikisha kuwa kuna usimamizi thabiti wa sheria hiyo na kanuni zake.

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu kwamba mipango si matumizi. Hivyo basi, katika kuimarisha matumizi sahihi ya fedha tunazozikusanya na kukopa tuliunda tena Tume ya Mipango ili kuhakikisha kuwa mipango ya kisekta inafungamana na malengo ya kitaifa pamoja na rasilimali tulizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumesimamia utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 kwa mafanikio makubwa. Uchumi umekua na nchi kuweza kuingia katika kipato cha kati, ngazi ya chini na kuimarisha maisha ya Watanzania. Serikali imekamilisha maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2050. Dira hiyo mpya tutakayoizindua rasmi mwezi Julai, mwezi unaofuata, itatupa mwelekeo utakaowezesha Taifa letu kupiga hatua zaidi za maendeleo. Niwashukuru wote waliohusika kuitayarisha, hususan wananchi walioeleza bayana mahitaji na matarajio ya Tanzania wanayotaka kuiona katika miaka 25 ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile ninafurahi kwamba tumefanya mazoezi yaliyoimarisha mfumo wetu wa takwimu au takwimu muhimu katika kufanya mipango yetu. Mwaka 2022 tulifanya Sensa ya Watu na Makazi, tukiendeleza utamaduni wetu wa kufanya sensa kila baada ya miaka 10. Vilevile tulifanya utafiti wa

mwenendo wa idadi ya watu na masuala ya afya. Zaidi ya hapo, na kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu tuliweza kufanya sensa ya majengo kote nchini. Mazoezi yote hayo yametuwezesha kupata taarifa muhimu zitakazotusaidia kupanga mipango yetu ya maendeleo kisayansi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, amani tuliyonayo kwa kiasi kikubwa inalindwa na uimara na ufanisi wa mahakama zetu na vyombo vingine vya kusimamia haki. Hii ni kwa sababu amani na utulivu hustawi pale ambapo haki huonekana kutendeka. Katika kuimarisha utawala wa sheria, kuongeza uwajibikaji, ufanisi na kupunguza malalamiko ya wananchi na ucheleweshaji wa mashauri, niliunda Tume ya Rais ya kuangalia namna ya kuboresha mifumo ya haki jinai. Mapendekezo ya Tume hiyo yanaendelea kutekelezwa na taasisi mbalimbali. Kwa kipindi chote mahakama imeendelea kuwa huru na kamwe Serikali haikuingilia mahakama katika kazi zake. Ili kuboresha utendaji na ufanisi wa mahakama tumeongeza bajeti ya mahakama kutoka shilingi bilioni 166.2 mwaka 2020/2021 mpaka kufikia shilingi bilioni 321 mwaka 2025/2026, sawa na ongezeko la 93%.

Mheshimiwa Spika, vilevile tumeongeza idadi ya majaji, Mahakimu na Mawakili wa Serikali, na nafarijika kwamba tumezingatia uwakilishi wa kijinsia. Katika kipindi hiki pia nimeteua majaji wapya 83 ambapo majaji wa Mahakama ya Rufani ni 15, kati yao wanne ni wanawake na majaji wa Mahakama Kuu 68, kati yao 30 ni wanawake. Ahsante. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, aidha, tuliwezesha ajira mpya ya Mahakimu na watumishi wengine jumla 1,153. Majaji na Mahakimu wanawake wamekuwa wengi wakati huu kuliko wakati mwingine wowote katika historia ya nchi yetu. Hatua hizi zimewezesha mahakama kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa pamoja na kuhakikisha kuwa mifumo ya TEHAMA katika utoaji huduma za kisheria inasomana na mifumo ya *NIDA*, TAKUKURU, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Jeshi la Polisi Tanzania na taasisi nyingine za kisheria.

Aidha, Serikali imeendelea kutekeleza Mpango wa Kutenganisha Shughuli za Mashtaka na Upelelezi kwa kuendelea kuongeza idadi ya mawakili wa Serikali na kuongeza ofisi za mashtaka za wilaya kutoka 50 hadi 108 ili kusogeza huduma za kisheria karibu zaidi na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mifumo ya utoaji haki, mafanikio mbalimbali yamepatikana, yakiwemo kukamilika kwa ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama sambamba na nyumba za kuishi Majaji zilizopo eneo la Iyumbu, Dodoma; ujenzi wa majengo ya mahakama za wilaya tatu na mahakama za mwanzo 26 katika maeneo mbalimbali nchini; ujenzi wa vituo sita jumuishi vya utoaji haki katika maeneo ya Dodoma, Morogoro, Mwanza, Arusha, Kinondoni na Temeke. Vilevile, kumekuwa ujenzi wa vituo tisa jumuishi vya utoaji haki katika Mikoa ya Katavi, Songea, Songwe, Njombe, Simiyu, Lindi, Singida, Pemba na Geita ambako nako ujenzi unaendelea. Miradi hii imewezesha kusogeza huduma za mahakama karibu na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha upatikanaji haki kwa watu wote Serikali imetekeleza Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia *(Mama Samia Legal Aid Campaign - MSLAC)*. Ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jumla ya wananchi 2,698,908 kwenye mikoa 25 wamepatiwa huduma mbalimbali za kisheria kupitia kampeni hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya pili katika historia ya nchi yetu, Serikali imekamilisha urekebu wa sheria kuu 446 za nchi na kuandaa Toleo la Sheria zilizofanyiwa Urekebu la mwaka 2023. Hatua hii inawarahisisishia watumiaji wa sheria zetu kufanya rejea ya sheria mbalimbali hususan wakati wa utoaji wa haki. Toleo hili ambalo litaanza kutumika tarehe 01 Julai, 2025 litaimarisha utawala wa sheria. Aidha, hadi sasa sheria kuu 300, kati ya 446, zimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili, hatua ambayo itaenda kuimarisha uelewa wa sheria miongoni mwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba yangu ya kufungua Bunge la Kumi na Mbili niliahidi kuifungua nchi kiuwekezaji ili kukuza uchumi, kuzalisha ajira, kuongeza mapato na kupunguza kiwango cha umaskini kitaifa na kwa mtu mmoja mmoja. Tunaendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini. Katika utekelezaji huu tulipitia na kurekebisha sheria na kanuni 66 pamoja na kufuta au kupunguza tozo, ada na faini mbalimbali zipatazo 383. Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* kimeweza kusajili jumla ya miradi ya uwekezaji 2,175 iliyopo kwenye sekta mbalimbali za uzalishaji na huduma. Miradi hiyo ina jumla ya thamani ya dola za Kimarekani bilioni 25.53 na inatarajia kuzalisha jumla ya ajira 650,674 za moja kwa moja na ajira nyinginezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jitihada za kuhamasisha uwekezaji katika maeneo maalumu ya kiuchumi *(SEZ)* pia zimevutia jumla ya miradi 45 yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 1.17 iliyopatiwa leseni za *EPZ* na *SEZ*. Miradi hiyo ilijikita katika sekta zinazozalisha bidhaa zitokanazo na kilimo, viwanda, mifugo, kemikali, madini na mazao ya misitu imeongeza ajira 20,674 na kuongeza ukuaji wa mauzo ya nje kwa dola za Marekani milioni 397.64. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuchochea uwekezaji nchini, tumetunga Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi ya mwaka 2025 ambayo pamoja na mambo mengine, inaanzisha mamlaka ya uwekezaji na maeneo maalum ya kiuchumi, kwa pamoja. Tumechukua kituo cha uwekezaji na maeneo maalum ya kiuchumi na kuyafanya pamoja na kutunga sheria moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilimo kimeendelea kuwa uti wa mgongo wa Taifa letu kwa kutoa ajira nyingi na kuchangia kwa kiasi kikubwa pato letu la Taifa. Kwa kutambua mchango wa sekta hii kwa maisha ya Mtanzania wa kawaida Serikali imeongeza bajeti ya kilimo kwa zaidi ya 300% kutoka shilingi bilioni 294 mwaka 2021 hadi shilingi trilioni 1.24 mwaka 2025. Shabaha yetu kuu ni kuongeza tija, pamoja na kuweza kujitosheleza kwa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza tija, Serikali imeongeza upatikanaji wa mbegu bora za kilimo kwa 41.9% kutoka tani 50,747 mwaka 2021 hadi tani 72,031.89 mwaka 2024. Aidha, uzalishaji wa mbegu bora ndani ya nchi umeongezeka kwa 61% kutoka tani 34,797 mwaka 2021 hadi tani 56,114 mwaka jana 2024. Pia tumewezesha maabara ya mbegu ya Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu kupata ithibati ya kimataifa ya uzalishaji wa mbegu. Hatua hii imewezesha uzalishaji mbegu bora unaoleta tija kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Serikali imeongeza upatikanaji wa mbolea kutoka tani 678,017 mwaka 2021 hadi tani milioni 1.21 mwaka 2025. Hii ni sawa na ongezeko la 80.9% ya makisio ya mahitaji ya tani milioni 1.5 za mbolea kwa msimu wa mwaka 2025. Sambamba na hilo, Serikali imetoa ruzuku ya mbolea yenye thamani ya shilingi bilioni 300 kwa mazao yote. Hatua hiyo, imewezesha kuongezeka kwa matumizi ya mbolea kwa hekta kutoka kilo 19 mwaka 2021 hadi kilo 24 mwaka 2025, na hivyo kuongeza tija kwenye uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali na mbolea Serikali pia imekuwa ikihakikisha upatikanaji wa viuatilifu pamoja na huduma za ugani kwa kuhakikisha inaajiri maafisa ugani pamoja na kuwapa vitendea kazi kama pikipiki, vishikwambi, visanduku vya ugani na *soil scanners* ili kuongeza tija kwenye kilimo chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tayari jitihada hizo za Serikali siyo tu zimemfaidisha mkulima, bali pia zimeongeza kiwango cha uzalishaji wa mazao ya chakula kwa 33% kutoka tani milioni 17.1 mwaka 2021 hadi tani 22.8 mwaka 2024. Ongezeko hilo limeiwezesha nchi kuwa na utoshelevu wa chakula kwa 128%. Pamoja na hayo, ili kulinda jasho la mkulima kwa kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno, tumejenga maghala 46 na vihenge 20 vyenye uwezo wa kuhifadhi mazao tani 219,921. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa maeneo mawili yaliyoibua mjadala kipindi hiki yalihusu sukari na mafuta ya kupikia au mafuta ya kula. Ili kuimarisha upatikanaji wa sukari

kunapokuwa na upungufu, tuliipa *NFRA* mamlaka ya kununua na kuhifadhi sukari kisheria. Hii ina maana kwamba sukari imeingia kwenye mazao ya usalama wa chakula ndani ya nchi. Ninawashukuru Wabunge kwa kuunga mkono mabadiliko hayo. Ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini tayari tumeshaanza kuona tofauti baada ya kuchukua hatua hizo. Pamoja na hayo, Serikali inaendelea na jitihada za kuongeza uzalishaji wa sukari nchini kwa kuhamasisha ujenzi wa viwanda. Mbali na kiwanda kipya cha Bagamoyo chenye uwezo wa kuzalisha sukari tani 35,000 na Mkulazi chenye uwezo wa kuzalisha sukari tani 50,000, upanuzi wa kiwanda cha Kilombero utaongeza uzalishaji wa sukari kwa tani 271,000.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, upanuzi umefanyika kwenye mashamba ya Mtibwa (hekta 4,700) na Kagera (hekta 9,071). Hadi sasa hatua hizi zimeongeza uzalishaji wa sukari kutoka tani 311,358 mwaka 2020 hadi tani 392,724 mwaka 2024. Tutaendelea kuvutia uwekezaji zaidi wa viwanda au kwenye viwanda na kupanua maeneo ya uzalishaji wa miwa tukilenga kufikia uzalishaji wa tani 700,000 za sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa msukumo pia katika kuongeza uzalishaji wa mafuta ya chakula. Hivyo, msukumo huo umewezesha uzalishaji mbegu za mafuta kuongezeka kutoka tani 1,713,178 mwaka 2021 hadi tani 2,181,603.65 mwaka 2024. Pamoja na hayo, uzalishaji wa mafuta ya kula nchini umefikia tani 396,335 tu. Hivyo, tunaendelea na hatua zitakazotuwezesha kuchochea uzalishaji zaidi wa mazao ya mafuta kuelekea lengo la tani 650,000. Aidha, tunadhamiria kuongeza usindikaji na uzalishaji wa mafuta ya kula nchini ili kupunguza uagizaji kutoka nje ambao kwa kweli unatugharimu fedha nyingi za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kilimo biashara, kuimarika kwa uzalishaji wa mazao ya biashara nchini kumeongeza thamani ya mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi kwa 67% kutoka dola za Kimarekani bilioni 2.1 mwaka 2021 hadi dola za Kimarekani bilioni 3.5 mwaka 2024. Pia uzalishaji wa

mazao asilia ya biashara umeongezeka kutoka tani 983,177 mwaka 2021 hadi tani 1,443,629.4 mwaka huu 2025. Tunacholenga ni kuongeza zaidi thamani ya mauzo nje ya nchi hadi kufikia dola za Kimarekani bilioni tano ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji maji ambapo eneo linalomwagiliwa limeongezeka kutoka hekta 561,383 mwaka 2020 hadi hekta 983,466.06 mwaka jana 2024. Hii inatokana na ongezeko la miradi ya umwagiliaji inayotekelezwa kutoka 13 mwaka 2020 hadi 780 mwaka huu 2025. Ni matumaini yetu kuwa kukamilika kwa miradi hii yote kutatuwezesha kufikia lengo tulilojiwekea la kufikia hekta 1,200,000 za eneo la umwagiliaji. Muhimu zaidi, katika jitihada hizi Serikali imeamua kutekeleza miradi mikubwa ya umwagiliaji maji kwa kutumia maji ya Ziwa Victoria na Tanganyika ambayo itaunda Gridi ya Umwagiliaji kwa ajili ya eneo lenye ukubwa wa hekta 3,000,000 ambapo ujenzi wake unatarajiwa kuanza ndani ya miezi 18 kuanzia sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali katika kukuza sekta hii imewezesha kutimia kwa azma ya muda mrefu ya kuimarisha ushirika kwa kuanzisha Benki ya Ushirika iliyoanza na mtaji wa shilingi bilioni 58. Kuanzishwa kwa benki hiyo ambayo wanahisa wakubwa ni vyama vya ushirika vyenyewe kunajibu hitaji kubwa na la muda mrefu la upatikanaji wa mikopo zaidi kwa gharama nafuu na hivyo kutaviwezesha vyama vya ushirika kujiimarisha kibiashara na kiuwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine kupitia mfumo rasmi wa manunuzi, kiwango kilichouzwa kupitia ushirika kimeongezeka kutoka tani 591,268.12 zilizouzwa kwa thamani ya shilingi trilioni 1.1 mwaka 2021 hadi tani milioni 2.23 zenye thamani ya shilingi trilioni 4.2 mwaka huu 2025. Ongezeko hilo linalokaribia 300%. Vilevile, Serikali iliiongezea mtaji Benki ya Maendeleo ya Kilimo *(TADB)* na hivyo kuongeza wigo wa upatikanaji wa mikopo nafuu kwa wakulima. Dhamana ya mikopo kwenye sekta ya kilimo imeongezeka kutoka shilingi bilioni 63 mwaka 2020, hadi shilingi bilioni 418.3 mwaka 2025, na tayari benki 19 zinatumia

Mfumo wa Dhamana wa Benki ya Kilimo kuongeza mikopo kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jitihada za kufungua masoko nje ya nchi, zimeongeza mauzo ya nyama kwa upande wa mifugo kutoka dola za Marekani milioni 4.2 mwaka 2020/2021, hadi kufikia tani 14,701 zenye thamani ya dola za Marekani milioni 61.4 mwaka huu. Tarehe 17 Juni mwaka huu, nilizindua Kampeni ya Kitaifa ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo inayolenga kulinda afya na kuongeza thamani ya mifugo yetu. Serikali katika kampeni hiyo itabeba nusu ya gharama ya chanjo ya mifugo ya ng'ombe na mbuzi, na gharama zote kwa kuku, na gharama zote za hereni za utambuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge katika maeneo yetu tuendelee kuhimiza matumizi bora ya ardhi kwa kuhamasisha watu wetu kutenga maeneo ya kilimo na ya ufugaji. Tuendelee kuhimiza vijiji vyetu kutekeleza mipango hiyo ili wafugaji wapate maeneo ya malisho mbali na mazao ya wakulima. Pia tuhimize uhamilishaji kama mlango wa kuingilia kwenye kuboresha kosafu za mifugo yetu. Ninadhani ni *species* za mifugo yetu au aina za mifugo yetu. Ni vyema kuhimiza watu wetu kuachana na uchungaji na kujikita katika ufugaji, lakini hapa ninataka ku-*quote quotation* maarufu ya Rais Kikwete kwamba huko nyuma na jitihada hizi zilianza wakati wa awamu yake na aliona kwamba mchungaji hanenepi, na mfugaji hanenepi wamo tu kwenye safari wanakwenda. Sasa tunataka kuwatoa wafugaji huko. Watoke kwenye uchungaji waingie kwenye ufugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maboresho katika sekta ya uvuvi yamechangia upatikanaji wa ajira za moja kwa moja kwa wavuvi 201,661, wakuzaji viumbe maji 49,084 na takribani Watanzania milioni sita wako katika shughuli mbalimbali zinazohusiana na uvuvi. Aidha, Serikali ilitoa mikopo iliyowezesha uwekezaji wa vizimba 1,636 na ununuzi wa boti 280. Vilevile, Serikali ilitoa boti 160 zenye thamani ya shilingi bilioni 11.51 ambazo zimetoa ajira 13,180. Kutokana na uwekezaji huo, mazao ya uvuvi yameongezeka kutoka tani 477,018 zenye thamani ya shilingi

bilioni 2.77 mwaka 2021, hadi kufikia tani 543,598.9 zenye thamani ya shilingi bilioni 3.04 mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha biashara ya mazao ya uvuvi ambapo mauzo yameongezeka kutoka tani 42,302 zenye thamani ya shilingi bilioni 412 mwaka 2021 hadi tani 59,749 zenye thamani ya shilingi bilioni 675 mwaka 2024. Tunaendelea na ujenzi wa bandari ya Kilwa Masoko ya uvuvi yenye thamani ya shilingi bilioni 279.5 ambao kwa sasa umefikia 81.9%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa bandari hiyo kunatarajia kuzalisha ajira takribani 30,000 na nchi kwa ujumla kunufaika zaidi na uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Spika, kwenye sekta ya ujenzi Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji ikiwemo kuongezeka kwa mtandao wa barabara za changarawe kutoka kilometa 24,493 mwaka 2020 hadi kilometa 44,372 mwaka 2025. Na mtandao wa barabara za lami kutoka kilometa 38,086.95 mwaka 2020 hadi kilometa 40,902 mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine yaliyopatikana ni kukamilika kwa ujenzi wa madaraja tisa ambayo ni Daraja la Gerezani na *Tanzanite* Dar es Salaam, Wami - Pwani, Kitengule - Kagera, Kiyegea - Morogoro, Ruaha - Morogoro, Ruhuhu - Ruvuma, Mpwapwa - Dodoma na Daraja la Msingi Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tumekamilisha ujenzi wa mradi wa kimkakati wa Daraja la John Pombe Magufuli. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine Serikali imetekeleza miradi ya kupunguza msongamano wa magari na foleni katika majiji. Tumekamilisha mradi wa miundombinu ya mabasi yaendayo haraka *(BRT)* awamu ya pili kilometa 20.3 Mbagala, Mzunguko wa Bandari, Bendera Tatu, halafu Bendera Tatu - Kariakoo, Sokoine, Zanaki, Barabara ya Kawawa na Barabara ya Morogoro - Magomeni na tunaendelea na utekelezaji awamu ya

tatu ya kilometa 23.3 kutoka katikati ya jiji hadi Gongo la Mboto ambayo imefikia 80% na awamu ya nne ya kilometa 30.1 kutoka katikati ya jiji hadi Tegeta ambayo imefikia 22%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi hii itakapokamilika itaongeza ufanisi na tija, tunaendelea kushughulikia changamoto na kasoro zilizopo katika mradi huu ili wananchi waweze kunufaika ipasavyo na usafiri huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia inaendelea na ujenzi wa barabara za mzunguko wa nje *(outer ring road)* katika Jiji la Dodoma lenye jumla ya urefu wa kilometa 112 ambapo utekelezaji kwa awamu zote mbili umevuka 80%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali inaendelea na upanuzi wa barabara kuu za Tanza sehemu ya Uyole, *Ifisi Songwe Airport* Jijini Mbeya yenye urefu wa kilometa 36 kutoka njia mbili kuwa njia nne ambapo ujenzi umefikia 23.5%. Miradi hii yote inaenda kuchochea shughuli za kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa viwanja vya ndege Serikali imekamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Nduli, Mkoani Iringa. Vilevile, inaendelea na ujenzi na ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Musoma ambapo ukarabati umefikia 58%, Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga ukarabati umefikia 60%, Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga ukarabati umefikia 80%, Kiwanja cha Ndege cha Tabora, ujenzi umefikia 93%, Kiwanja cha Ndege cha Kigoma ujenzi umefikia 20% na Kiwanja cha Ndege cha Geita ujenzi umefikia 80%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato hapa Dodoma sehemu ya kwanza inayohusisha ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege *(run way)* barabara za maungio *(tax ways)* na maegesho ya ndege umefikia 87%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili inayohusisha ujenzi wa jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, kituo cha zimamoto na kituo cha hali ya hewa, ujenzi umefikia 53.2%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi hii itafungua zaidi anga la Tanzania kuchochea shughuli za kiuchumi na kuongeza fursa za biashara ikiwemo mazao ya mbogamboga, matunda na maua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa reli, niliahidi Bunge hili kuwa nitakamilisha ujenzi wa reli Dar es Salaam hadi Dodoma na kuendelea na ujenzi wa vipande vingine. Nafurahi kusema kuwa kama mnavyojua awamu zote mbili Dar es Salaam - Morogoro, Morogoro - Dodoma tayari zimekamilika na reli inatembea. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, ahsante, tangu safari za reli hii kuanza mwezi Agosti, 2024 tayari jumla ya abiria milioni 254,828 wamesafiri na maduhuli ya shilingi bilioni 60.88 yamekusanywa. Kuanza kwa huduma za usafiri wa reli hiyo kumeongeza tija kwenye uchumi kwani kimefupisha safari ya Dar es Salaam na Dodoma toka saa nane hadi tisa hadi saa tatu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa imekuwa kawaida na ninyi ni mashahidi naambiwa mnalala Dar es Salaam na mnaamka Dodoma hapa asubuhi. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa vipande vingine vya *SGR* unaendelea ambapo kipande cha kutoka Mwanza - Isaka kilometa 341 umefikia 63.16%. Makutupora - Tabora umefikia 14.53%, Tabora - Isaka umefikia 6.65% na Tabora - Kigoma umefikia 7.81%. Aidha, maandalizi ya kuanza ujenzi wa kipande cha Uvinza - Malagarasi - Musongati kinachounganisha Tanzania na Burundi yameanza na tunatarajia kuzindua ujenzi hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutekelezwa kwa mradi huu wa *SGR* kumezalisha ajira 9,376 hizo ni za moja kwa moja pamoja na

kampuni zaidi 792 za Watanzania kusaini mikataba kwa ajili ya mkandarasi na huduma mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imenunua mabehewa ya mizigo 264 ambapo kazi ya majaribio ya mifumo imefanyika. Nafurahi kuwajulisha Bunge kwamba leo ni siku ya kihistoria kwenye reli yetu ya *SGR* kwa kuwa Shirika la Reli limeanza rasmi safari za mizigo kati ya Dar es Salaam hadi Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatarajia hatua hii ya kimageuzi nchini itapunguza muda na gharama ya uchukuzi kuchochea biashara na kuimarisha nafasi ya Tanzania kama lango la biashara katika Afrika ya Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo Serikali inaendelea na uboreshaji wa reli ya kati iliyokuwepo awali yaani *Meter Gauge Railway (MGR)* ambayo inaendelea kutoa huduma kwa njia ya kati na Kaskazini sambamba na reli ya *SGR*. Katika kutekeleza azma hiyo tumenunua vichwa vya treni vitatu, mabehewa ya abiria 22 na ya mizigo 44. Vilevile, jumla ya mabehewa 350 ya mizigo na 33 ya abiria yamekarabatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika utoaji wa huduma za usafiri wa anga niliahidi kuwa tutaendelea kuiboresha kampuni yetu ya ndege ya *ATC* kimkakati ili iweze kujiendesha kwa ufanisi. Katika kipindi hiki Serikali imenunua ndege sita za abiria na moja ya mizigo na hivyo kufanya *ATCL* kuwa na jumla ya ndege 16 hadi Aprili ,2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa ndege hizo umesaidia nchi kuwa na usafiri wa anga wenye uhakika ingawa bado tunasuasua, lakini tulipo siko tulipotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *ATC* pia inatarajia sasa kutanua safari zake ndani ya Bara la Afrika na nje ya Bara la Afrika. Tunatarajia kuongeza safari kwenda Nigeria, Msumbuji, Oman na Angola. Ununuzi wa ndege ya mizigo imepunguza hasara kwa wazalishaji na kujenga mtangamano wa uzalishaji wa ndani na soko la kimataifa. Vilevile, kuimarishwa kwa *ATC* kumekuwa kichocheo

cha ukuaji wa sekta nyingine ikiwemo utalii na kumesaidia katika kuitangaza nchi yetu kimataifa. Hivyo, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha tunafanya jitihada za makusudi ili *ATCL* iweze kuimarika zaidi na kujiendesha kwa tija.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bandari, maboresho ya bandari zetu za Tanzania na ushirikishwaji wa sekta binafsi kwenye uendeshaji wa baadhi ya gati imewezesha kupunguza wastani wa muda wa meli kusubiri nangani, umepungua kutoka siku 46 hadi siku saba. Muda wa meli za makasha kusubiri nangani umepungua kutoka siku tano na sasa huingia moja kwa moja gatini pindi zinapowasilia katika Bandari ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, idadi ya makasha inayohudumiwa imeongezeka kwa 35% kutoka makasha 159,807 hadi makasha 215,286 na jumla ya uzito wa shehena iliyohudumiwa imeongezeka kwa 14% toka shehena tani milioni 14,424 hadi tani milioni 16,870.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji uliofanywa umeongeza makusanyo ya mapato ya Serikali hususan yale yanayotokana na kodi toka wastani wa shilingi milioni 850 kwa mwezi kwa mwaka 2023/2024 hadi shilingi trilioni moja kwa mwezi mwaka 2024/2025 na umepunguza matumizi kwa Shirika la Bandari kwa mwezi kutoka wastani wa shilingi bilioni 262 kati ya mwezi Mei, 2023 na Machi, 2024 hadi shilingi bilioni 169. Imetoka shilingi bilioni 262 hadi 166,323,000,000 kati ya mwezi Mei, 2024 hadi Machi, 2025.

Mheshimiwa Spika, pia tunaendelea kufanya maboresho katika bandari zetu za Mtwara na Tanga. Uboreshaji wa Bandari ya Mtwara uliohusisha ujenzi wa gati, uzio na barabara inayounganisha gati jipya na maeneo mengine katika bandari umekamilika. Hatua hiyo imesaidia wananchi wa Mtwara na maeneo ya jirani kuongeza biashara na uwekezaji pamoja kuharakisha usafirishaji wa mizigo kwa gharama nafuu hususan mazao ya korosho, ufuta na makaa ya mawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na uboreshaji wa bandari zilizopo katika Bahari ya Hindi, Serikali pia imeendelea kuongeza wigo wa huduma za kibandari kwa kujenga na kuboresha bandari zilizopo katika maziwa makuu nchini. Kazi kubwa zilizofanyika ni pamoja kukamilisha uboreshaji wa Bandari ya Kemondo, kuendelea na uboreshaji wa Bandari ya Bukoba ambao umefikia 94% na Bandari ya *Mwanza North* ambao umefikia 58%.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha ukarabati wa boti MV Tangazo iliyopo Tanga pamoja na mategenezo ya boti MV Mkongo iliyopo Pwani ambazo zimeanza kutoa huduma. Vilevile, tunaendelea na ukarabati mkubwa wa vivuko vingine ambao umefikia hatua tofauti. MV Kilombero II, MV Nyerere, MV Oduruvu, MV Magogoni, MV Ukara, MV Kigamboni na MV Pangani II vipo katika hatua tofauti za matengenezo.

Mheshimiwa Spika, pia tunaendelea na ujenzi wa vivuko vipya sita kama ifuatavyo; Bwiro-Bukondo, Kisoria - Rugezi, Iringa - Kahangara, Nyakaliro - Kome, Buyangu - Mbalika na Nyamisati - Mafia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza katika Ziwa Victoria unakamilika ndani ya muda mfupi. Pamoja na juhudi hizi…*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru niliongea sana kule Mozambique kwa hiyo, sauti imegoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasema pamoja na juhudi hizi Serikali inakaribisha sekta binafsi kuwekeza katika maeneo ya vivuko nchini.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Serikali imefanikiwa kuongeza mtandao wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kutoka kilometa 8319 hadi 13,820 sawa na ongezeko la 66%. Kuongeza wilaya zilizounganishwa na mkongo toka wilaya 36 mwaka 2020 hadi

wilaya 109 hivi sasa na kukamilisha vituo 111 vya kutolea huduma za mkongo wa mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imepunguza gharama za *internet* na kupiga simu ndani na nje ya nchi. Vilevile, minara ya mawasiliano imeongezeka kutoka 754 mwaka 2020 hadi kufikia minara 9,278 mwaka 2025. Minara hiyo imewezesha upatikanaji wa mawasiliano kwenye maeneo yenye changamoto na kuchagiza maendeleo ya uchumi kupitia biashara mtandao.

Mheshimiwa Spika, vilevile kadri matumizi ya mifumo ya kidigitali inavyokuwa kwenye kila sekta ndivyo kumeongezeka haja ya kujipanga kuhakikisha mageuzi ya kidigitali yanatuletea faida au fursa zaidi. Ni kwa msingi huo tuliandaa mkakati wa uchumi wa kidigitali wa miaka kumi 2024/2034 na mkakati wa Taifa wa *broadband* 2021/2026 inayolenga kujenga miundombinu wezeshi ya kidigitali na kuweka sera rafiki ya uchumi wa kidigitali, kuimarisha ujuzi wa masuala ya kidigitali na kukuza utamaduni wa ubunifu miongoni mwa watu wetu.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa wadau muhimu katika ubunifu tunapojenga uchumi wa kidigitali ni kampuni changa maarufu kama *startups* hususan kwenye eneo la TEHAMA. Kipindi hiki Serikali imeimarisha mashauriano na wadau wa sekta hii na kimekuwa kinasisitiza kuwa inataka kuona Serikali inazisaidia *startups* ili vijana watumie ujuzi huo kuongeza tija kwenye shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kukuza kampuni hizo za vijana Serikali itatunga sera kuendeleza kampuni changa *(startup policy)* aidha tutaendeleza miradi ya ubunifu *(innovations)* 464 iliyotokana na mashindano ya kitaifa ya sayansi, teknolojia na ubunifu au MAKISATU, na tumeanzisha Mfuko wa Bunifu ujulikanao kwa jina la *Mama Samia Innovation Fund* ili kuwezesha utoaji wa mikopo nafuu kwa wabunifu, kuanzisha kampuni na kuingiza bidhaa sokoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa sekta ya madini,

tumeimarisha masoko na minada ya uuzaji wa madini ambapo vituo vya ununuzi wa madini vimeongezeka kutoka vituo 61 Novemba, 2020 hadi 109 mwaka huu, masoko ya madini yameongezeka kutoka 41 hadi 43, *either* Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imeanzisha viwanda vya usafishaji dhahabu kwa kiwango cha kimataifa katika Mikoa ya Mwanza, Dodoma, Dar es Salaam, Geita na Chunya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tumeendelea kuimarisha Shirika la Taifa la Madini *(STAMICO)* kama nilivyoahidi ili kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za madini. Serikali pia imesimamia sekta hii na kuiwezesha kuongeza mchango wake katika pato la Taifa kutoka 6.8% mwaka 2020 hadi kufikia 10% mwaka huu, lakini kwa habari njema tulifikia mwaka jana 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tumetekeleza ahadi ya kuwaendeleza wachimbaji wadogo kwa kununua mitambo ya uchorongaji iliyosambazwa katika maeneo ya Tambi – Mpwapwa, Nyawa – Bariadi, Matondo – Makongorosi na Matundasi yalioko Chunya; Rwamgasa – Nyaruyeye – Nyamalimbe na Nyakagwe yaliyopo Geita. Pia Mavota – Biharamulo, Endabash – Karatu, Mwakitoja – Shinyanga na Mbangala – Songwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha Serikali imefuta leseni za maombi 2,648 ili kuwawezesha wachimbaji wadogo kupata maeneo halali ya uchimbaji ili wazidi kuimarika. Kwa sasa mchango wa wachimbaji wadogo umefikia 40% ya mapato yote yatokanayo na sekta ya madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua mahsusi ili kuhakikisha sekta ya maliasili na utalii inakua zaidi na kuongeza mchango wake kwenye Pato la Taifa. Hatua hizi zimechangia kuongeza idadi ya watalii wa kimataifa kwa 132.1%, kutoka watalii 922,692 mwaka 2021 hadi watalii 2,141,895 mwaka jana 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile idadi ya watalii wa ndani imeongezeka kwa 307.9% kutoka watalii 788,933 mwaka 2021 hadi kufikia watalii 3,218,552 mwaka 2024. Hatua hii imewezesha vijana

wengi wa Kitanzania kupata ajira za moja kwa moja kwenye sekta ya utalii katika vituo na kufungua kampuni zao binafsi za utalii. Idadi wa wakala wa biashara za utalii zimeongezeka kutoka 2,885 mwaka 2020 hadi 3,735 mwaka 2025. Kwa idadi ya waongoza watalii imeongezeka kutoka 5,076 mwaka 2020 hadi 7,662 mwaka huu 2025. Vilevile mapato yatokanayo na utalii yamepanda kutoka dola za Kimarekani milioni 700 mwaka 2020 hadi dola za Marekani bilioni 3.9 mwaka 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa watalii wa kimaitafa, mapato yameongezeka kutoka shilingi bilioni 46.3 hadi shilingi bilioni 209.8 kwa watalii wa ndani katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, tarehe 01 Desemba, 2024 katika Jiji la Arusha nilifanya mkutano na wawakilishi wa wakazi wa eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, mazunguzo yale yaliangazia masuala makubwa mawili, matumizi ya ardhi na haki mbalimbali na pili changamoto zilizojitokeza wakati wa zoezi la uhamaji wa hiyari kwa wakazi wa eneo hilo kwenda eneo la Msomera, Wilaya ya Handeni – Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mkutano huo nilipata fursa ya kusikiliza malalamiko yao pamoja na kupata maoni na ushauri wao juu ya njia bora zaidi ya kushughulikia suala la uhamaji wa wakazi wa eneo hilo. Kwa kuwa malalamiko yalikuwa mengi na mazito niliamua kuunda Tume mbili, kuangalia kwa kina suala hili kwa lengo la kupata suluhu ya kudumu. Tume hizo mbili zinatathimini masuala ya ardhi na zoezi la uhamaji kwa hiyari na zitakuja na mapendekezo kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuendelea kuimarisha utawala na usimamizi wa ardhi, Serikali imeboresha Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 itakayosaidia kuboresha sekta hiyo muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu. Ni matarajio yetu kuwa kila kipande cha ardhi nchini kitapimwa na kumilikishwa kihalali kwa shughuli za kiuchumi na kijamii ili kuondoa matumizi holela na kuondoa migogoro ya ardhi. Vilevile tutaimarisha mamlaka za utatuzi wa migogoro hii na kuongeza matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Novemba, 2020 hadi Aprili, 2025 jumla ya hatimiliki 356,642 zimesajiliwa. Hati za Hakilimiki za Kimila 318,868 zimetolewa kwa wananchi na kukamilisha upimaji na uidhinishaji wa viwanja 1,427,005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha Serikali imeendelea kutumia mfumo wa kieletroniki wa ardhi katika kutoa hatimiliki, hatua hizo zimeimarisha usalama wa ardhi, utambuzi wa kisheria wa umiliki wa ardhi, kuondoa migogoro ya ardhi na kuongeza thamani na usalama wa ardhi yetu. Ili kuondoa migogoro ya ardhi Serikali inajipanga kuanzisha Tume ya Ardhi ili kuimarisha usimamizi wa ardhi nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa sekta ya nishati kwa maendeleo ya nchi, niliahidi kuwa Serikali itaimarisha upatikanaji wa nishati nchini, hasa kwa kukamilisha ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere na kufikisha umeme kwenye vijiji vyote. Nafurahi kulitaarifu Bunge kwamba msukumo uliotolewa na Serikali umewezesha ongezeko kubwa la uzalishaji wa umeme kutoka megawati 1,601.84 mwaka 2020 hadi megawati 4,031.71 mwaka huu. Ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali hii imechangiwa na ukamilishaji wa miradi mbalimbali ya uzalishaji na usambazaji umeme ikiwemo mradi wa kielelezo wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji wa Julius Nyerere wenye megawati 2,115. Vilevile miradi mingine iliyokamilika katika kipindi hiki ni mradi wa kuzalisha umeme wa *Kinyerezi Extension MW 185* kwa kutumia gesi asilia na Mradi wa Rusumo ambao umetekelezwa katika Mto Kagera kwa kushirikiana na nchi tatu za Tanzania, Burundi na Rwanda kwa mgawanyo sawa wa umeme wa megawati 26.67 kila nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imekamilisha miradi ya usambazaji umeme, ikiwemo miradi wa ujenzi wa njia za usafirishaji umeme wenye urefu kilometa 414 kutoka Singida hadi Arusha – Namanga, kilometa 144 kutoka Geita – Nyakanazi, Njia ya Julius Nyerere hadi Chalinze, Njia ya Nyakanazi hadi Kigoma, Njia ya kilometa 115 kutoka Tabora – Urambo, Njia ya kilometa 94

kutoka Rusumo – Nyakanazi na kwenye njia ya Reli *(Standard Gauge Railway)*. Mafanikio hayo yameongeza upatikanaji wa nishati ya umeme ya uhakika katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, tumefanikiwa kuiunganisha Mikoa ya Kigoma na Katavi kwenye Gridi ya Taifa ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kama tulivyoahidi tumefikia hatua kubwa na ya kihistoria kwenye usambazaji kwa kuweza kupeleka umeme kwenye vijiji vyote 12,318 vya Tanzania Bara kama tulivyoahidi. Kwa sasa tunaendelea na kazi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji ambapo tayari vitongoji 33,657 kati ya 64,359 vimeshafikiwa na umeme, sawa na 52.3%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali pia ina mpango wa kuzalisha nishati mbadala kupitia vyanzo jadidifu, lakini pia hivi karibuni wakati namuapisha Mkurugenzi Mtendaji wa *TANESCO* nilimwelekeza umuhimu wa kuanza kuzalisha nishati ya umeme kwa kutumia nyuklia. Ahsante. *(Makofi)*

Aidha, tunapanga kuweka ushindani kwenye sekta ya nishati kwa kualika sekta binafsi kushiriki kuongeza upatikanaji wa umeme wa uhakika na nafuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua mbalimbali kuimarisha utendaji kazi kwa mashirika ya umma ili kuongeza mchango wake katika kujenga uchumi. Tulifanya mapitio na uchambuzi kuhusu uendeshaji wa mashirika na taasisi za umma 248 ili kuongeza tija na mchango wa mashirika hayo katika kuleta maendeleo. Matokeo ya tathmini hiyo yamewezesha Serikali kuanza zoezi la kuunganisha baadhi ya mashirika na taasisi kurekebisha muundo wa mashirika na taasisi za umma na hivyo kuimarisha usimamizi, kuongeza uwekezaji na kujiendesha kwa faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maboresho hayo pia yamewezesha Serikali kuongeza makusanyo ya gawio na michango kwa mwaka kutoka shilingi bilioni 691.6 mwaka 2021 hadi shilingi trilioni 1.028 mwaka 2025. Ongezeko la shilingi bilioni 336 kwa mwaka zinazoenda kuboresha huduma kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeboresha sera, sheria na programu mbalimbali ili kuweka mazingira bora ya kuwawezesha wananchi kiuchumi. Vilevile mfuko wa programu na programu mbalimbali zimeboreshwa ikiwemo Mipango ya Kunusuru Kaya Maskini *(TASAF),* mipango ya mikopo ya 10% ya mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya wanawake, vijana na wenye ulemavu. Programu ya Jenga Kesho Iliyobora *(BBT)*, Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi kwa Vijana, Programu ya Kukuza Viwanda Vidogo na Vya Kati, Programu ya Imarisha Uchumi na Mama Samia; Mfuko wa Dhamana wa Wajasiriamali Wadogo, Mfuko wa *SELF Microfinance* na Mpango wa Kutenga 30% ya Manunuzi ya Taasisi za Umma kwa Wazabuni Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu. Mifuko na programu hizo zimetoa zaidi ya shilingi trilioni 3.68 na kuwanufaisha zaidi watu milioni 24. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini - Awamu ya Tatu inayotekelezwa katika maeneo yote Tanzania Bara na Zanzibar. Idadi ya wanufaika imeongezeka kutoka kaya 876,440 mwaka 2021 hadi kaya 1,371,916 mwaka 2025. Vilevile jumla ya fedha zilizohawilishwa kwa walengwa katika kipindi hiki ilifikia shilingi trilioni 1.15. Kupitia fedha hizo jumla ya miradi 27,863 yenye thamani ya shilingi bilioni 291.7 ilitekelezwa na kaya 909,440 kufikia mwaka 2025 ikilinganishwa na miradi 3,185 yenye thamani ya shilingi bilioni 38.6 na kaya 197,110 kwa mwaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaliahidi Bunge kuwa tutaimarisha na kukuza uhusiano na mataifa mengine pamoja na jumuiya za kikanda na za kitaasisi za kimataifa. Tangu mwaka 2021 tulipata fursa ya kuwapokea viongozi mbalimbali wa kimataifa waliotutembelea na sisi kufanya ziara kwenye nchi rafiki kwa lengo la kuimarisha uhusiano na ushirikiano. Ziara hizo zimeimarisha mahusiano, kutufungulia masoko na kutuongezea misaada na mikopo yenye masharti nafuu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Sekta ziklizonufaika zaidi ni pamoja na nishati, kilimo, mazingira, uchukuzi, afya, elimu, biashara na uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kutokana na ziara hizo ni pamoja na kuongeza fursa ya masoko kwa mazao yetu mbalimbali. Kwa mfano mwaka jana Tanzania iliondolewa ushuru wa forodha kwa 100% kwa bidhaa zote zinazozalishwa nchini kwenda soko la China. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna miradi mbalimbali tuliyonufaika moja kwa moja na ushirikiano huo ikiwemo mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya upimaji wa ramani na mradi wa ujenzi wa vyuo vinne vya ufundi na mafunzo ya mali katika Mikoa ya Kigoma, Mwanza, Mtwara na Zanzibar. Nchi yetu itaendelea kuimarisha uhusiano na ushirikiano na mataifa mengine duniani ili kuendelea kunufaika na fursa zinazopatikana kwa mashirikiano hayo. Tumetembelewa na wageni kutoka mataifa mbalimbali makubwa ikiwemo Marekani, Ujerumani, Indonesia pamoja na Wakuu wa Taasisi za Kimaitafa ikiwemo Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika na mimi na wasaidizi wangu, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu pamoja na Naibu Waziri Mkuu tumefanya ziara kwenye Mabara ya Ulaya, Marekani, Afrika, Asia na Mashariki ya Kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imevutia mikutano mikubwa nchini ikiwemo Mkutano wa Nishati Barani Afrika, Mkutano wa Afrika kuhusu Rasilimali Watu na Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika iliyoiwezesha Tanzania kuchangia kutoka utatuzi wa changamoto zinazolikumba bara letu. Vilevile Tanzania imekuwa mwenyeji wa mikutano mbalimbali ya kikanda ikiwemo hiyo iliyolenga kutafuta amani Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ambapo kwa mara ya kwanza tulifanikiwa pia kufanya mkutano ulizozileta pamoja Jumuiya mbili za kikanda yaani Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya *SADC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuimarika kwa nafasi yake kimataifa, Tanzania ilipata heshima ya kushiriki majukwaa mbalimbali kwa mara ya kwanza na kuchangia mwelekeo wa Sera za Ushirikiano wa Kimataifa, ikiwemo Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa *G20* na Mkutano wa *BRICS* hatua iliyokuza zaidi ushawishi wetu kimataifa. Kupitia majukwaa haya pamoja na mengi mengine tuliweza kutoa msukumo kwa ajenda ya

upatikanaji wa nishati safi ya kupikia kwa ajili ya kulinda mazingira na afya za watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki Tanzania ilishika nafasi mbalimbali za kikanda na Tanzania ilichaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika kwa vipindi viwili na sasa ni Mwenyekiti wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC)* ambapo tulipata fursa ya kusimamia chaguzi kadhaa ikiwemo za Msumbiji, Namibia, Botswana na Mauritius. Pia tumo kwenye Kamati Tendaji ya Umoja wa Afrika ambayo mwaka 2028 tutachukua Uenyekiti wa Umoja huo na hivyo kwa mara ya kwanza umoja huo utatoa Mwenyekiti Mwanamke, *Inshallah.* Ahsante, tuombe Mwenyezi Mungu atufikishe salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, tulipata fursa ya kuchangia misheni za ulinzi wa amani nchini *DRC* na Msumbiji chini ya *SADC*. Majukwaa yote haya yaliiwezesha Tanzania kuchangia katika jitihada za kuimarisha amani na utulivu katika bara letu. Aidha, Watanzania mbalimbali walichaguliwa kushika nafasi za kimataifa, ikiwemo mtu wetu maarufu Profesa Mohamed Janabi, aliyechaguliwa kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nililiahidi Bunge kwamba tutaimarisha utendaji kazi wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ikiwa ni pamoja na Balozi zetu. Hivyo, pamoja na kuajiri watumishi wapya (ajira 148) kwenye Wizara na kupeleka watumishi katika Balozi zetu zote 128 na niliahidi watarudi kwa wakati na mwaka huu tuna mpango wa kuwarudisha na kupeleka wapya *(exchange)*. Ule mtindo wa maafisa kukaa ubalozini mpaka anaitwa bibi tunataka kuuacha na sasa watakwenda miaka minne anarudi kituoni anakwenda kituo kingine miaka minne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile niliunda Tume ya Rais ya kutathmini Utendaji wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambayo iliwasilisha ripoti na mapendekezo ambayo tunaendelea kuyatekeleza. Moja ya mapendekezo

ambayo tumekamilisha ni Uzinduzi wa Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001, Toleo la 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sera hiyo ina lengo la kuhakikisha mikakati yetu inajibu mazingira ya sasa. Vilevile, tumechukua hatua ya kuirejeshea hadhi ya Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim, maarufu kama Chuo cha Diplomasia. Vilevile tumeanzisha Balozi mpya katika nchi za Austria na Indonesia, na Konseli Kuu za Guanzghou – Jamhuri ya Watu wa China na Lubumbashi – Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Hatua hiyo imefanya nchi yetu kuongeza balozi zake kutoka 43 hadi 45 na konseli tatu hadi tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kupitia diplomasia tumeweza kushawishi nchi zifuatazo kufungua Konseli Kuu na Konseli za Heshima Zanzibar. Nchi hizo ni *UAE* (Konseli Kuu) na zilizofungua Ofisi za Uwakilishi wa Heshima ni Ufaransa, Uingereza, Italia, Ujerumani, Hispania, Sweden, Brazil na kuchochea fursa za biashara, utalii na uwekezaji hususan katika sekta ya uchumi wa buluu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha tumenunua majengo ya ubalozi nchini Namibia, ukarabati wa majengo ya Ubalozi nchini Ubelgiji, Sweden na ujenzi wa Balozi zetu katika nchi ya Kenya. Katika kuboresha utendaji wa Wizara tumeweka Katibu Mkuu anayesimamia Masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Naibu Waziri. Vilevile, tumeunda Idara ya Diplomasia ya Uchumi pamoja na Idara ya Mikakati ya Siasa za Ulimwengu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia maboresho ya Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001, Toleo la mwaka 2024, tunalenga kurahisisha ushirikishwaji wa wana-*diaspora* (Watanzania walioko nje). Hatua zote hizi nilizozitaja kuhusu masuala ya kiuchumi kwa pamoja zimechangia jitihada za Serikali kuongeza fursa za ajira nchini kupitia uwekezaji katika sekta mbalimbali, ambapo kwa kushirikiana na sekta binafsi, katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025, jumla ya ajira 8,084,204 zimezalishwa. Tutaendeleza jitihada

hizi kwani nguvu kazi kubwa tuliyonayo ni mtaji mkubwa wa kusukuma maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kutambua mchango wa mtumishi wa umma katika maendeleo na ustawi wa Taifa letu, Serikali imechukua hatua mbalimbali kuboresha maisha yao. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha mifumo ya ushughulikiaji wa maslahi ya watumishi wa umma, kuwajengea uwezo, pamoja na kuwapatia vitendeakazi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki, jumla ya watumishi wa umma 611,063 wa kada mbalimbali wamepandishwa vyeo, 42,557 wamebadilishwa kada zao na 9,620 wamefanyiwa mabadiliko ya mshahara binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kipindi hiki watumishi wapya 135,626 wameajiriwa katika taasisi mbalimbali za umma. Aidha, Serikali imeendelea kulipa jumla ya shilingi bilioni 252.76 za malimbikizo ya mishahara na maslahi ya watumishi 150,647, na shilingi bilioni 33.29 za malimbikizo ya mishahara ya wastaafu 10,022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Serikali imeongeza mshahara wa kima cha chini kutoka shilingi 370,000 hadi shilingi 500,000 sawa na ongezeko la 35.1%. Aidha, imetoa ajira katika taasisi mbalimbali za umma kwa watumishi 135,626. Vilevile, jumla ya nafasi za ajira 155,008 zilitolewa na vibali vya ajira mbadala, ambapo 41,673 vilitolewa ili kujaza nafasi zilizobaki wazi kwa sababu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa kutumia Mtandao wa Mawasiliano Serikalini *(GovNet),* vituo vya Serikali vya kuhifadhia mifumo, *data* na masafa ya intaneti ili kuondoa urudufu, kupunguza gharama, kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa kwa umma pamoja na kuhakikisha uwepo wa usalama wa mawasiliano Serikalini. Sasa mifumo ya taasisi mbalimbali za umma inabadilishana taarifa baada ya kujenga mfumo mkuu wa kuiwezesha mifumo ya TEHAMA Serikalini kubadilishana taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, kufuatia msisitizo wangu wa kutaka mifumo ya Serikali kusomana, eneo lingine ambalo tumefanikiwa ni kuunganisha mifumo ya Serikali 898 ya kutolea huduma. Kati ya hiyo, mifumo 514 ni ya Serikali na mifumo 384 ni ya sekta binafsi. Uunganishaji wa mifumo umeongeza ufanisi katika utoaji na upatikanaji wa huduma za Serikali kwa umma kupitia Serikali mtandao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jitihada za Serikali yetu zimeifanya Tanzania kutambuliwa kimataifa katika matumizi ya TEHAMA Serikalini ambapo kwa mujibu wa utafiti wa Benki ya Dunia kuhusu ukomavu wa matumizi ya teknolojia duniani, nchi yetu imepanda daraja kutoka Kundi B hadi Kundi A katika utoaji wa huduma za Serikali na ushirikishwaji wa wananchi. Hivyo, tumeshika nafasi ya kwanza kwa upande wa nchi za Afrika Mashariki, ya pili Barani Afrika na nchi ya 26 duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile katika kuimarisha usalama wa taarifa za watu, tumeanzisha Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya mwaka 2022, pamoja na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi inayosimamia utekelezaji wake. Sheria hiyo imewezesha uwepo wa usalama na faragha ya taarifa za mtu, watu au taasisi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa Mfumo wa Utambuzi wa Anwani za Makazi katika kurahisisha mawasiliano, utoaji, upokeaji wa huduma, ufikishaji na ufanyaji wa shughuli za kijamii, kiuchumi na kiutawala, nilielekeza mfumo huo ukamilishwe kwa njia ya *operation*. Ninashukuru Serikali ilifanya kazi hiyo na kwa sasa, taarifa za anwani za makazi ziliongezeka kutoka 350,000 mwaka 2020 hadi 12,853,657 mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miundombinu ya anwani za makazi, vibao vya namba vya nyumba vimeongezeka kutoka 300,125 mwaka 2020 hadi 7,440,812 mwaka huu. Vilevile nguzo za majina ya barabara zimeongezeka kutoka 9,842 mwaka 2020 hadi 229,961 mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuzungumzia huduma za kijamii, niruhusu nianze na sekta ya elimu; pamoja na kuendeleza kazi nzuri ya ujenzi wa miundombinu katika sekta ya elimu, Serikali imeboresha Sera ya Elimu ya mwaka 2014 Toleo la 2024 na mitaala ya elimu katika ngazi ya elimu ya awali, msingi, sekondari na elimu ya ualimu ili kuimarisha utoaji wa elimu katika ngazi hizo na kujielekeza kutoa elimu ujuzi kulingana na mazingira ya nchi na mahitaji ya soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imeongeza bajeti ya sekta ya elimu kutoka shilingi trilioni 4.72 mwaka 2020/2021 hadi shilingi trilioni 6.16 mwaka 2024/2025 iliyosaidia kuimarisha miundombinu pamoja na kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundishia. Pamoja na mambo mengine, Serikali imejenga shule 26 za sekondari za sayansi za wasichana kwa kila mkoa, shule saba za sekondari za wavulana za sayansi kila kanda na shule 103 za sekondari za mafunzo ya amali na ufundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imeongeza vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari kutoka madarasa 191,708 mwaka 2020 hadi 254,393 mwaka 2025. Aidha, Serikali imeboresha shule 274 za michepuo ya kilimo na shule 28 za michepuo ya biashara, imetoa vifaa vya kisasa katika shule 28 za mchepuo wa elimu ya ufundishaji amali na imekamilisha ujenzi wa nyumba 1,792 za walimu, maabara 638, maktaba 1,128 na mabweni 1,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza mpango wa elimu bila ada kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha sita, na imeongeza bajeti ya mpango huo kutoka shilingi bilioni 312.06 mwaka 2020 hadi shilingi bilioni 796.58 mwaka jana 2024. Hatua hiyo imewezesha kuongezeka kwa wanafunzi wanaonufaika na mpango huo kutoka 14,940,925 mwaka 2020 hadi 16,155,281 mwaka 2024. Vilevile, katika kuhakikisha kila Mtanzania anapata fursa ya elimu iliyo bora, Serikali imewarejesha shuleni wanafunzi 18,347 waliokatiza masomo kutokana na sababu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza falsafa ya "Asiachwe Mtu Nyuma" katika elimu kwa kuandaa Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi Nchini wa mwaka 2021/2022 - 2025/2026. Mkakati huo utaboresha mazingira na utoaji wa elimu jumuishi kwa kuongeza nafasi ya mafunzo kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum pamoja na kukamilisha ujenzi wa shule jumuishi za mfano zikiwemo Lukuledi - Mkoani Mtwara, Shule Maalum ya Sekondari Patandi - Mkoani Arusha na Shule Jumuishi ya Mfano ya Awali na Msingi na Sekondari Mbuye iliyopo Mkoani Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza msisitizo kwenye ujuzi, Serikali imeongeza vyuo vya ufundi stadi kutoka 662 mwaka 2020 hadi 860 mwaka 2024 yaani ongezeko la vyuo 198. Jitihada hizo zimeongeza udahili katika vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi kutoka wanafunzi 344,815 mwaka 2020 hadi 446,521 mwaka 2025. Vilevile, imekamilisha ukarabati wa vyuo 10 vya *VETA* na sita vya ufundi stadi na huduma za utengamao wa watu wenye ulemavu katika Mikoa ya Tanga, Tabora, Singida, Dar es Salaam na Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tumeanzisha vituo vya umahiri hususan katika sekta za nishati, kilimo na usindikaji, usafirishaji, TEHAMA na viwanda vya uzalishaji vilivyopo katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeongeza mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kutoka shilingi bilioni 464 mwaka 2020 hadi shilingi bilioni 787.4 mwaka 2025. Kutokana na hatua hii, idadi ya wanufaika na mikopo ya elimu ya juu imeongezeka kutoka wanafunzi 142,170 mwaka 2020 hadi wanafunzi 248,332 mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, programu ya ufadhili inayojulikana kama *SAMIA Scholarship* imeanzishwa na hadi sasa imewafundisha jumla ya wanafunzi 1,343 waliojikita kwenye masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi, hesabu na afya. Zaidi ya hapo, tumeanza kutoa mikopo kwa wanafunzi wa ngazi ya stashahada wanaosoma fani za kipaumbele zikiwemo afya, sayansi na ufundi ambapo shilingi bilioni 19.95 zimetolewa kwa

wanafunzi 7,534. Vilevile Serikali iliondoa tozo ya 6% kulinda thamani ya fedha kwenye mikopo ya wanafunzi wa vyuo vya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kujenga vituo vya kutolea huduma za afya kwenye sekta ya afya, kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaatiba, kuongeza upatikanaji wa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi, kutoa mafunzo kwa wahudumu wa afya na kuhamasisha matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kuongezeka kwa vituo vya kutolea huduma za afya kutoka vituo 8,783 mwaka 2020 na kufikia vituo 12,846 mwaka 2025, sawa na ongezeko la vituo 4,063. Ongezeko hilo limesogeza huduma za afya karibu zaidi na wananchi ambapo sasa inakisiwa kwamba 75% ya wananchi wanapata huduma za afya ndani ya kilometa tano ya maeneo wanayoishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nililieleza Bunge kuwa tutaendeleza kampeni ya "Jiongeze Tuwavushe Salama" ili kuhamasisha uwajibikaji wa wadau wote katika kupunguza vifo vya mama na mtoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa majengo ya kutoa huduma za afya ya mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda-Meta iliyopo katika Jiji la Mbeya iliyogharimu shilingi bilioni 13.2 na ambayo tayari inatumika, pamoja na Hospitali za Rufaa za Mikoa za Sekou Toure - Mwanza, Geita, Simiyu, Mawenzi, Njombe na Songwe ambazo zimegharimu kiasi cha shilingi bilioni 71.1. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile vituo vyenye uwezo wa kutoa huduma za upasuaji wa dharura wa kumtoa mtoto tumboni vimeongezeka kutoka vituo 340 mwaka 2020 hadi vituo 577, pamoja na wodi. Kumeongezeka pia wodi au vyumba maalum kwa ajili ya magonjwa ya watoto wachanga. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeongeza hospitali zenye majengo ya kutolea huduma za dharura kutoka saba mwaka 2020 hadi 125 mwaka 2025. Kukamilika kwa majengo ya kutolea huduma za dharura kumepunguza vifo na kuokoa maisha ya wagonjwa wa dharura na wa ajali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imeimarisha huduma za uchunguzi kwa kununua vifaatiba vya uchunguzi ambavyo vinapatikana kuanzia ngazi ya Hospitali ya Taifa hadi Hospitali za Rufaa za Mikoa na Halmashauri. Vifaa tiba vilivyoongezeka ni pamoja na *MRI* kutoka saba hadi 13, *CT scan* kutoka 13 hadi 45, *Digital X-Ray* kutoka 147 hadi 491 na *Ultrasound* kutoka 476 hadi 970. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa dawa na vifaatiba aina 382 katika vituo vya umma imeongezeka kutoka 73% mwaka 2020 na kufika 86.2% Aprili, 2025. Upatikanaji wa dawa, vifaatiba na vitendanishi unawezesha wananchi kupata mahitaji muhimu ya msingi katika vituo vya kutolea huduma za afya. Kutokana na kuimarika kwa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi, kumekuwa na ongezeko la utaliitiba kwa wagonjwa wanaohitaji huduma hizo kutoka nje ya nchi kutoka 5,705 mwaka 2020 hadi 12,180 mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huduma za kibingwa na ubingwa bobezi zinazotolewa ni pamoja na uwekaji wa vifaa vya usikivu kwa watoto, upandikizaji wa figo, kuweka puto tumboni, upasuaji mgumu wa moyo bila kufungua kifua na upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua. Pia upasuaji ubongo, upasuaji wa uti wa mgongo, upandikizaji wa nyonga bandia na tiba ya saratani ya mlango wa kizazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utafiti wa viashiria na matokeo ya VVU na UKIMWI umeonesha kuwa tumefanikiwa kuvuka lengo kwenye utekelezaji wa shabaha ya 95% ya pili inayohusisha tiba kwa watu wenye VVU waliotambua hali zao ambapo 98% wapo kwenye tiba. Pia utafiti katika shabaha ya tatu inayohusu kufubaza virusi vya WAVIU wanaoendelea na tiba unaonesha kwamba 94% ya

waliopo kwenye tiba ndio wamefubaza. Kwa hiyo, tunaendelea vizuri na waliofubaza maana yake hawaambukizi.

Mheshimiwa Spika, katika kufikia shabaha ya kwanza inayohusu watu wote wanoishi na VVU kupima na kujua hali zao za maambukizi, 82.7% ya watu wanoishi na VVU nchini sasa wanajua hali zao. Pamoja na kupungua kwa baadhi ya misaada ya wabia wetu kutokana na mabadiliko ya sera zao, Serikali imejipanga kuhakikisha kuwa haturudi nyuma katika kufikia shabaha... *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, Serikali itahakikisha kuwa haturudi nyuma katika kufikia shabaha iliyowekwa kimataifa ya 95-95-95. Afya za Watanzania zitabaki kuwa kipaumbele cha kwanza cha Serikali na uwekezaji stahiki utafanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kutimiza azma ya upatikanaji wa maji safi na salama, kama ilivyoelekezwa kwenye Ilani ya CCM, Serikali imetekeleza mikakati na programu mbalimbali ikiwa ni pamoja na miradi ya usambazaji maji 2,331 mijini na vijijini.

Aidha, miongoni mwa miradi mikubwa iliyotekelezwa ni pamoja na ifuatayo: -

(i) Mradi wa Kuboresha Huduma ya Maji katika Miji 28 ya Tanzania Bara kwa gharama ya shilingi trilioni 1.3, ili kunufaisha wananchi wapatao 5,985,500;

(ii) Mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira wa Arusha uliogharimu zaidi ya shilingi bilioni 520 na ambao umeongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 40 hadi lita milioni 200 kwa siku.

(iii) Mradi wa muda mrefu wa Same – Mwanga – Korogwe uliogharimu shilingi bilioni 406.1 na kunufaisha zaidi ya wananchi 456,930; na

(iv) Mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka Vijiji ya Tinde na Shelui, ujenzi wa chujio la Butimba, mradi wa Mugango – Kiabakari – Butiama na ule wa Orkesumet ambao umegharimu zaidi ya shilingi bilioni 200.86 na kunufaisha wananchi wapatao 1,048,910 na mifugo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha uwezo wa utekelezaji wa miradi ya maji, Serikali imenunua mitambo 25 ya kuchimba visima; seti tano za mitambo ya kuchimba na kujenga mabwawa na seti nne za vifaa vya uchunguzi wa maji ya ardhini. Mitambo hiyo imewezesha uchimbaji wa visima 1,749 na ujenzi wa mabwawa 16 katika maeneo mbalimbali nchini na hivyo, kuwawezesha wananchi kupata maji kwenye maeneo ya karibu na makazi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha ujenzi wa mabwawa 45 kwa ajili ya uvunaji wa maji ya mvua ili kuwezesha upatikanaji wa maji hata wakati wa kipindi cha ukame. Vilevile, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi mkubwa wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda litakalokuwa na uwezo wa kutunza lita bilioni 190 za maji. Mradi huo utakaogharimu shilingi bilioni 329.46 umefikia 29% na utapokamilika utasaidia kupunguza athari za kimazingira kwa kuimarisha utiririshaji wa maji katika mkondo wa Mto Ruvu kwa kipindi chote cha mwaka, kuwezesha mitambo ya kuzalisha maji ya Ruvu Juu na Chini ili kupunguza changamoto ya upatikanaji wa maji katika Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla jitihada za Serikali katika sekta ya maji zimewezesha hali ya upatikanaji wa maji mijini kuongezeka kutoka 84% hadi 91.6% na vijijini kutoka 70.1% hadi 85%. Aidha, kuna miradi kadhaa inayoendelea na utekelezaji mijini na vijijini ambayo ikikamilika kwa sehemu kubwa itatuwezesha kutekeleza azma yetu ya kumtua mama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, nafurahi kulijulisha Bunge kwamba tumekamilisha maboresho ya Sera ya Taifa ya Maji ya

mwaka 2002, Toleo la mwaka 2025, tukilenga kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maji, kuimarisha utoaji huduma ya maji safi na usafi wa mazingira vijijini, kujipanga vizuri zaidi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuboresha uratibu wa mipango wa pamoja kwa sekta zinazotekeleza miradi inayohusiana na maji yaani hapa ni sekta ya maji na sekta ya kilimo wawe na mipango ya pamoja kwenye ujenzi wa mabwawa na pia umwagiliaji. Hatua hizi zitazidi kuwahakikishia wananchi upatikanaji wa maji safi na salama wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Kinga ya Jamii ya mwaka 2023 ambayo imeweka uratibu madhubuti na kuimarisha utekelezaji wa afua stahiki za kinga ya jamii. Utekelezaji wa sera hiyo pamoja na afua nyingine umesaidia kuongeza idadi ya wanachama wachangiaji kutoka 849,886 mwaka 2021 hadi 1,758,018 mwaka 2025. Vilevile, ulipaji wa mafao kwa wastaafu umeboreshwa kwa kufanya mabadiliko ya kikokotoo.

Mheshimiwa Spika, maboresho hayo yameongeza wigo wa malipo ya mkupuo kutoka 33% hadi 40% kwa waliokuwa wanalipwa 50% kabla ya kuunganisha mifuko mwaka 2018 na kutoka 33% hadi 35% kwa waliokuwa wanapata 25%. Aidha, Serikali imeongeza kima cha chini cha pensheni kutoka shilingi 100,000 hadi shilingi 150,000 kwa mwezi na kuhuisha pensheni ya kila mwezi kwa kiwango cha asilimia mbili kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sanaa; kufuatia maboresho yaliyofanywa na Serikali kiasi cha mirabaha kilichogawiwa kwa wasanii waliosajiliwa *COSOTA* kimeongezeka kutoka shilingi milioni 245 hadi shilingi milioni 687.7 na hivyo kuwezesha wasanii kupata fedha na kunufaika na kazi zao za sanaa. Vilevile, vibali vya wasanii wa ndani kwenda nje ya nchi kufanya shughuli za sanaa vimeongezeka kutoka 122 hadi 1,492 na vibali vilivyotolewa kwa wadau kuingiza wasanii nchini kufanya shughuli za sanaa kutoka 75 hadi 623. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa michezo; mafanikio mbalimbali yamepatikana na kubwa ni Tanzania kufanikiwa kwa mara ya kwanza kuwa mwenyeji wa matukio makubwa ya michezo ya Kimataifa ya *AFCON* mwaka 2027 na *CHAN* kwa mwaka huu wa 2025. Vilevile, vilabu vyetu ya mipira vya miguu vikubwa vya Simba, Yanga, Azam na vingine, na Namungo Waziri Mkuu, lakini kwenye ninalolisema Namungo haimo, vimeweza kufuzu kushiriki mashindano ya Shirikisho la Soka la Afrika *(CAF)*. Tunawapongeza sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio niliyoyabainisha si kwamba hakuna changamoto, bado zipo na zinaendelea kushughulikiwa. Kama nilivyosema awali, maendeleo ni hatua, hivyo basi tunaendelea kuifanyia kazi mipango na mikakati mbalimbali ili kuhakikisha tunapunguza umaskini kwa kutumia rasilimali zetu, kuongeza uwajibikaji Serikalini, kupunguza matumizi yasiyo na tija na kupunguza utegemezi. Ni matumaini yangu kuwa mpaka mwaka 2030 nchi itakuwa imefikia uchumi wa kati kiwango cha juu. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, tunaamini na ni matumaini yetu kwamba wananchi watatupa ridhaa kupitia uchaguzi ujao ili tuweze kuendeleza jitahada za kuwaletea wananchi maendeleo endelevu. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha nisisitize kwamba utendaji wa Serikali unapimwa kwa tathmini na takwimu. Mimi nimetumia takwimu katika uwasilishaji wangu kueleza utekelezaji wa ahadi zetu kwa wananchi. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, nashukuru.

*(Hapa baadhi ya Wabunge Waliimba Wimbo Tuna Imani na Samia)*

**WABUNGE FULANI:** Tuna imani na Samia,
Oyaa oyaa oyaaa,

Tuna imani na Samia
Oyaa oyaa oyaa,
Samia kweli, kweli, kweli Samia
Rais wetu, kweli, kweli, kweli kweli Samia. *(Makofi)*

**MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN – RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge.

Nilikuwa nasema, mimi nimetumia takwimu kusema yaliyotendeka katika kipindi hiki cha miaka minne. Ninyi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi na mmeyaona yaliyotendeka kwenye maeneo yenu. Mwenye macho haambiwi tazama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapoelekea kuhitimisha na kwa moyo mkunjufu nirudie kuwashukuru Watanzania wenzangu, kuanzia wakulima, wafugaji, wavuvi, wafanyabiashara, wafanyakazi wa sekta za umma na binafsi na hata wanasiasa kwa kuiunga mkono Serikali. Watanzania tumeendelea kudhihirisha uungwana wetu hususan kwa kudumisha amani, mshikamano, kuchapa kazi kwa bidii na kwa moyo wa uzalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa kipekee, nawashukuru viongozi wenzangu wote wa Serikali tulioshirikiana katika kipindi cha miaka minne. Namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango - Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa ushauri na ushirikiano alionipa katika kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa spika, namshukuru pia Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi - Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na viongozi wengine wa SMZ kwa ushauri na ushirikiano walionipa. Vilevile, namshukuru na kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. Ahsante. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hekima, unyenyekevu na uchapaji kazi mzuri. Aidha,

ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu. Namshukuru kwa kumsaidia Waziri Mkuu na kwa usimamizi wake wa sekta ya nishati. Nyote ahsanteni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, vilevile natoa pia shukrani zangu kwa Katibu Mkuu Kiongozi, Mheshimiwa Balozi Dkt. Moses Kusiluka, kwa kufanya kazi kwa bidii na weledi na kujitoa kwake bila kuchoka. Pia ninawashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kufanya kazi kwa jitihada kubwa sana. *(Mkaofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri. Nawashukru Maafisa Tarafa, Watendaji wa Kata na Vijiji pamoja na viongozi wa ngazi zote kwa kufanikisha kupatikana kwa mafanikio yote niliyoyataja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shukrani nyingi kwa wasaidizi wangu wa Ofisi Binafsi ya Rais na kwa upande mwingine naishukuru sana nguzo ya matumaini yangu. Hakika, bila maliwazo kutoka familia yangu kazi hii isingekuwa nyepesi. Ahsante. *(Makofi/Vigelegele)*

Hivyo nawashukuru kwa kunielewa kwa kutokuwa nao kwenye shughuli muhimu za kifamilia na kiukoo, mimi nikiwa mke, mama, dada, shangazi na bibi pia walikuwa wananikosa na nimewafanya wanangu wakue na wabebe majukumu badali yangu, kwa hiyo ninawashukuru wote kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninakishukuru chama changu, Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, CCM. *(Makofi)*

**MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN - RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ninakishukuru kwa kusimamia vyema Serikali na kuhakikisha kuwa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2025 inatekelezwa ipasavyo. Ninapenda kuwaahidi wanachama, wapenzi wa CCM na

wananchi kwa ujumla kuwa tumejipanga kutekeleza ilani ijayo kwa kaulimbiu ya "Kazi na Utu, Tunasonga Mbele." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninavishukuru pia vyama vyote vya siasa kwa ushirikiano wao kwa Serikali katika kipindi hiki cha miaka minne. Licha ya tofauti zetu za kisiasa na kiitikadi ukweli ni kuwa sote ni Watanzania na tunajenga Taifa moja. Wengi waliokuwa wakitukosoa au wakiikoso Serikali kwa nia ya kujenga sio kupinga tu kila lililokuwa likifanywa na Serikali walikuwa wakisaidia kuboresha utendaji wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru viongozi wa dini nchini kwa sala na dua zao za kuliombea Taifa letu na kutuombea sisi tuliokabidhiwa dhamana ya kuliongoza Taifa hili. Aidha, niwashukuru wanahabari kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya ya kutoa taarifa na kuelimisha umma wa Watanzania pamoja na dunia nzima kwa ujumla kuhusu masuala mbalimbali ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu nivishukuru sana vyombo vya ulinzi na usalama. Amani tunayojidai nayo leo ni kwa sababu vyombo vyetu vipo kazini, kwa hiyo, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine ninarudia kulishukuru Bunge lako la Kumi na Mbili kwa ushirikiano mkubwa lililoutoa kwa Serikali katika kipindi cha miaka hii tuliyofanya pamoja. Mbali na kuishauru na kuisimamia Serikali, Bunge hili ndilo lililopitisha bajeti na miswada mbalimbali ya sheria iliyowezesha Serikali kutimiza majukumu yake kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia nitumie fursa hii kuwashukuru washirika wa maendeleo, wadau wetu wa maendeleo mbalimbali kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia. Ushirikiano wao ulitupa nguvu na ari ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hivyo basi tunawashukuru sana washirika wetu wa maendeleo ambao kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri wa Fedha, wakati akiwasilisha hotuba yake ya Bajeti ya Serikali, aliwataja mmoja baada ya mwingine na mchango wao

umetambuliwa na kuingia kwenye *Hansard* za Bunge hili. Washirika wetu ahsanteni sana, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilianza kusema kuwa nimekuja kulihutubia Bunge na kuhitimisha shughuli za Bunge hili la Kumi na Mbili ili kuruhusu kuanza kwa mchakato wa uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani utakaofanyika Oktoba, 2025. Uchaguzi ni zoezi la Kikatiba na lenye umuhimu katika kukuza demokrasia nchini na kuwapa wananchi fursa ya kuchagua viongozi wanaowataka. Katika hilo ninatambua kuwa baadhi yenu hapa mmeonesha nia kuwania tena nafasi zenu na pia wapo waliotangaza kukaa pembeni, kama kaka yangu Mheshimiwa George Mkuchika, eeeh! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yeye amekwishasema, mimi jamani imetosha nakaa pembeni. Sasa kwa wanaoendelea niwatakie kila la kheri, niwatakie kila la kheri na ninajua mambo yamekuwa vizuri, lakini msisahau, Chalamila yupo, Chalamila yupo, kwa hiyo mwende mkafuate sheria na kanuni zote za uchaguzi, ninawatakia kila la kheri. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Serikali tumejipanga kuhakikisha kuwa uchaguzi unakuwa huru na wa haki na Serikali itakuwa macho kipindi chote kusimamia sheria na utulivu wa nchi. Ninarudia Serikali, dola itakuwa macho kipindi chote kusimamia sheria na utulivu wa nchi. Nitumie fursa hii kuhimiza vyama vyote vya siasa kutoa fursa za kutosha kwa wagombea wanawake, vijana ...*(Makofi)*

Haya, ahsante, ahsante, ahsante, ahsante, ahsante, ninataka nilirudie hilo.

Mheshimiwa Spika, ooh, wanawake wana fujo. *(Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Tuna imani na Samia, oyaaa, oyaaa, oyaaa.

**MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN - RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mheshimiwa Spika, ninawashukuru ....

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Oktoba, tunatiki.

**MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN - RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Wabunge, lakini mmeingia haraka wanawake.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka kusema, kutoa fursa za kutosha kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kugombea nafasi tofauti za uwakilishi. Vilevile niwasihi wagombea kuepuka matusi, vurugu au vitendo ambavyo haviendani na mila na desturi zetu kama Watanzania. Kama nilivyosema, tubishane kwa hoja na tushindane kwa ilani zetu, kamwe tusiruhusu uchaguzi uwe chanzo cha kuvuruga amani, bali tuhakikishe inakuwa nyenzo ya kuimarisha amani, utulivu na demokrasia nchini. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na kwa mamlaka niliyonayo chini ya Ibara ya 90(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, sasa ninayo heshima kutamka kuwa shughuli za Bunge la Kumi na Mbili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimehitimishwa na Bunge litavunjwa rasmi tarehe 3 Agosti, 2025. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, ahsante...

**MBUNGE FULANI:** Chalamila amesikia mwezi wa nane.

**MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN - RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, mnashangilia kuendelea kuitwa Waheshimiwa Wabunge, sivyo? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema Mungu libariki Bunge letu la Tanzania, Mungu wabariki Wabunge wote, Mungu aibariki nchi yetu Tanzania.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Kazi Iendelee.

**MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN - RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mheshimiwa Spika, ahsanteni sana kwa kunisikiliza, ahsante sana. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Oktoba, tunatiki.

**SPIKA:** Ahsanteni sana, ahsanteni sana.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kumshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuja hapa Bungeni na kutueleza sisi kwa niaba ya wananchi wote utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, lakini pia utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo.

Mheshimiwa Rais, tunakushukuru sana kwa kazi kubwa ambayo umeifanya, sisi maneno yetu mengi ya kutambua mchango wako mkubwa ulioufanya katika haya yote uliyoyasema, pamoja na kwamba umeshirikiana na viongozi wengine wa Serikali kama ulivyosema, lakini pia umetambua mchango wa Bunge katika maendeleo haya, sisi tulishazungumza yale ambayo tulitaka tukwambie kuhusu kazi nzuri unayoifanya, leo hatutayarejea hayo. Kwa hiyo, tunakushukuru kwa haya maelezo uliyotupa leo ambayo yanathibitisha kwamba tuzo tuliyokupa Mheshimiwa Rais, ulistahili na unastahili zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, kwa kusema hivyo, niungane nawe, Wabunge hawa kila mmoja wengine kupitia vyama vyao, wengine kupitia milango mingine isiyo ya vyama vyao, lakini wanakwenda kugombea. Yale makofi aliyokuwa anapigiwa Ndugu Chalamila ni kuashiria kwamba kule ulinzi uimarike ili hawa Wabunge wasiwe hatarini. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Rais, utekelezaji huu wa mpango wa maendeleo wa miaka mitano uliotuletea hapa ndio ambao Wabunge hawa watautumia kwenda kusema maendeleo

yaliyofanyika katika halmashauri zao, katika majimbo yao, katika wilaya zao, katika mikoa yao na pia katika Taifa lao. Kwa hiyo na mimi ninawatakia kila la heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais, kipekee na mimi niungane nawe kumuaga rasmi Kepteni Mstaafu Mheshimiwa George Huruma Mkuchika, tunakutakia kila la kheri katika maisha ambayo yatakuwa nje ya Bunge, Mwenyezi Mungu akutangulie. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa kusema hivyo uchaguzi ni vita, lakini twende huko basi tukafanye yale ambayo Mheshimiwa Rais ametuagiza. Sina shaka kwamba wengi wetu tutatumia yale ambayo ameyafanya Mheshimiwa Rais, tukijinasibisha nayo kwa sababu sisi ndio tuliokuwa tunapitisha hapa bajeti, utekelezaji wa hayo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais, baada ya shukrani hizi kwa wewe kuzungumza nasi na kwa kututajia tarehe ya mwisho ya Bunge hili, basi kwa mujibu wa Katiba yetu, Ibara ya 90 ambayo Mheshimiwa Rais utatumia hiyo kuliitisha Bunge baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, basi nami naahirisha shughuli za Bunge mpaka Mheshimiwa Rais atakapoitisha Bunge kupitia hiyo Ibara ya 90 ya Katiba yetu. Kila la kheri Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Haya, sawa, sasa Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

*(Hapa Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Ziliimbwa)*

*(Saa 2.28 Usiku Bunge la Kumi na Mbili Liliahirishwa Rasmi hadi hapo Litakapoitishwa Tena)*